

TUONYESHE BABA ITATUTOSHA



...?...Na tuendeleo kusimama kwa muda kidogo tu kwa ajili ya maombi, huku tukiinamisha vichwa vyetu.

² Baba mwenye Neema nyingi na Mtakatifu, tunapokikaribia kiti Chako cha Kiungu cha neema, tunasimama katika vivuli vya haki Yako. Tungeomba, Bwana, ya kwamba kwa neema Yako kwamba ungetusamehe dhambi na makosa yetu. Tunatamani rehema, usituhukumu kulingana na maisha yetu na matendo yetu, usitupe haki, lakini utupe rehema.

³ Baba, tunaomba ya kwamba utafanya hii a—alasiri ambayo itakumbukwa kwa muda mrefu kwa sababu ya Uwepo Wako. Tukikushukuru Wewe kwa yale ambayo umefanya asubuhi ya leo kote mjini, na kote bondeni, na kote ulimwenguni. Twaomba, Mungu, ya kwamba utaendelea kuwa pamoja nasi, na kutupa neema Yako na rehema mpaka Yesu atakapokuja. Bariiki Maneno yatakayosomwa na ma—maelezo yatakayotolewa juu ya Neno. Roho Wako na awe katika yote tufanyayo ama tusemayo. Waponye wagonjwa na wanaoteseka.

⁴ Wala hatutasahau, Bwana, wale wanaopata afueni, wale wasioweza kuja. Tunaomba ya kwamba Roho Mtakatifu atasimama karibu na kitanda chao alasiri ya leo, wakati wengi humu jengoni wanapowabebea mizigo, jalia waponywe.

⁵ Maisha yatakapokwisha nasi tusimame katika Uwepo Wako tutainama, kwa unyenyekevu, kukushukuru na kukupa Wewe sifa zote. Kwa kuwa tunaomba, katika Jina la Yesu. Amina.

⁶ Mwaweza kuketi. Ni furaha sana kuja na kuzungumza na kusanyiko katika Jina la Bwana Yesu, tukiwa na hakikisho hili, ya kwamba Yeye—Yeye hatatuacha wala kutupungukia, atakuwa pamoja nasi katika kila jaribu tulilo nalo. Na imani nyenyekevu tu ya kumwamini, kumkubali kama Mwokozi wetu, na kumwamini Yeye kwa yote tunayohitaji maishani.

⁷ Najua kuna joto sana alasiri ya leo, lakini mngeshangaa ni tofauti jinsi gani hapa na ilivyo katika Kongo ya Ubelgiji, ambako wangekuja, na huko chini Afrika Kusini, wangekuja asubuhi, nao wangekaa uwanjani siku nzima kwenye jua hilo lenye joto na linalosababisha malengelenge, si kwa siku moja tu, bali kungojea kule kwa majuma mawili ama matatu nipate kuingia nchini.

⁸ Wanashuka kupitia misituni, wakiwabeba wapendwa wao kwenye mbao, na kadhalika, simba angekuja, nao wangewasukuma juu ya mti, na kungoja labda siku nzima, ama, mpaka huyo simba aondoke, kisha washuke chini. Labda waende mbele kidogo, wajaribu kunywa maji yanayoteremka,

mamba angemnyakua mmoja wa hao watoto, wangeendelea kusonga mbele. Mnaona? Wania kwa saa chache, wanajua imekwisha, kisha wanaendelea mbele. Hao ni watu, hawajali joto, wanajaribu kupata uhai, mnaona, wanajaribu kupata *Kitu fulani* kinacholeta amani, na, kinachopita ufahamu.

⁹ Basi alasiri ya leo, hebu na tuudumishe huo, uaminifu mkubwa sana, niani mwetu tunapoketi alasiri ya leo. Najua kuna joto, lakini hatuwezi kutawala hali ya hewa. Hatuna budi kuwa na hali ya hewa yenye joto ipate kuzaa tunda, na kadhalika, Mungu anajua jinsi ya kuiandaa dunia Yake i—ilete wingi tupate kuishia. Na kama tungekuwa na mvua yote, na vivuli, na kadhalika, tungekufa kwa njaa. Kwa hiyo, tunashukuru sana kuwa hapa. Nami naona watu wana feni mkononi mwako, sasa, kama mna umeme, mbona, itakuwa sawa basi, itasaidia kupoza kidogo.

¹⁰ Sasa, hebu na tuliendee Neno kwa Yohana Mtakatifu, mlango wa 14. Kuanzia kesho usiku, Bwana akipenda, ningependa kuzungumza mfululizo wa masomo yanayojenga imani nikiweza. Mungu atanisaidia. Ninataka kujaribu kujenga imani kwa ajili ya ibada zijazo juma hili lijalo. Jaribuni, mkiweza, najua wengi wenu mnaifanya kazi, na ni vigumu kutoka.

¹¹ Si—si lazima nininii . . . nitake kusema hili kusudi mje, ninii tu, mara nyingi matamshi hayo yanatolewa, natumaini sivyo, kamwe haijawahi kuwa hapa, mara nyingi watu wanataka umati mkubwa wa watu wapate matoleo fulani. Mara nyingi wanataka umati mkubwa wa watu ujitokeze kwa ajili ya matokeo ya kisaikolojia uliyo nayo kwa watu, kwamba, watu wengi husema, “Vema, sitaki kuhubiri, isipokuwa kuwe na umati mkubwa.”

¹² Nilihubiria umati mkubwa na umati mdogo, haiteti tofauti ni upi. Ndio kwanza nifanye uamsho katika kanisa lililoenea watu ishirini. Kwa hiyo, ulikuwa ni wa kusikitisha, huko chini katika hali ya hewa sufuri, nao walikuwa wamesimama nje. Lakini sihitaji pesa, inatubidi tu kulipia matumizi, hivyo tu ndivyo mnavyoombwa kufanya. La—laiti ningaliweza kuyalipia mimi mwenyewe, nisingeomba hiyo.

¹³ Nami si—sikuchukua sadaka maishani mwangu. Ninakumbuka wakati mmoja, ambao nilikuwa, nilifikia mahali pagumu. Ni wangapi wanaojua hiyo inamaanisha nini? Mke wangu ameketi hapa alasiri ya leo, kwa kawaida huona haya kidogo, aliniangalia niliposema jambo hili, lakini ndiyo kwanza niingie kutoka, nilikuwa nikifanya kazi . . . Nilikuwa mchungaji wa maskani huko Jeffersonville kwa muda wa miaka kumi na saba na kamwe sikupata hata senti moja ya mshahara, licha ya hayo niliweka pesa ambazo ningeweza kuweka akiba katika ma—matoleo, na sikuzote nililipa zaka zangu, na kadhalika.

¹⁴ Lakini niliingia, na sisi hatukuwa na pesa za kutosha kufanya kitu hicho kiende, ndipo nikamwambia, nikasema, “Unajua nini, Mpenzi? Nitachukua sadaka usiku wa leo.”

Akasema, “Ninataka kuhakikisha kwenda kule na kukuona ukifanya hivyo.” Na kwa hiyo, akaketi hapo nyuma.

¹⁵ Sasa, watu wangetoa. Ulikuwa ni wakati wa vita, na kadhalika, na, ama, kabla tu ya vita. Na kwa hiyo, a—alijua ya kwamba wangetoa. Wange—wangepunguzia watoto wao chakula wapate kunisaidia, lakini ni—ni—nilitambua jambo hilo, wala kamwe sitaki kujinufaisha na kitu kama hicho.

¹⁶ Kwa hiyo, nilikuwa kijana, nikifanya kazi, nilikuwa mahali ambapo ningeweza kufanya kazi, na nilikuwa na kazi ya doria, nikitembea maili thelathini *na kitu* kwa siku kupitia nyikani, na kadhalika, ngumu sana, nikipata senti arobaini na tano kwa saa.

¹⁷ Lakini basi ni—nikaenda kule kuchukua sadaka, na kamwe sitasahau hilo, rafiki yangu wa kale, nikasema, “Marafiki, kidogo nina haja usiku wa leo,” nikasema, “ninahitaji yapata dola tano.” Nikasema, “Nina bili inayofaa kulipwa, siwezi kuilipa,” nikasema, “nina vitu vingine.” Nikasema, hatukuwa na sahani ya sadaka kanisani, nikasema, “Kama mtu mmoja atachukua kofia yangu *pale*, tutachukua tu sadaka, ukiwa na ndururu, ama chochote kile, pamoja.” Lilikuwa ni kusanyiko linaloenea sakafu hii, kanisa langu. Nami nikasema . . .

¹⁸ Bw. Wiseheart akaenda pale kuichukua kofia yangu, nami nikaangalia na maskini mwanamke mmoja mkongwe, maskini bikizee, mmoja wa akina mama wa mtindo wa kale waliokuwa wakivaa maskini aproni hizi zenye madoadoa, na zilikuwa na mfuko kwa ndani, mwajua, ya hiyo aproni. Mliwahi kuona moja ya hizo?

¹⁹ Nyanya yangu mkongwe, alikuwa akivaa moja ya hizo, naye alivuta kiko cha mwanzi. Hakutaka wanaume wamwone akivuta sigara, kwa hiyo alibeba tumbaku yake kwenye mfuko huo, naye angewaona baadhi ya wanaume wakija, angeingiza tu mkono wake chini ya hiyo aproni, huku kidole gumba chake kimekishikilia kiko chicho, kisha anazunguma nao. Baada ya wao kuondoka, angevuka sakafu, kiko hicho cha kale cha mwanzi.

²⁰ Ninakumbuka, kabla hajafa (Alikuwa na umri wa miaka mia moja na kumi, alikumbuka mauaji ya Abraham Lincoln, kamwe hakuona ila gari moja maishani mwake, nililileta hilo huko chini, huko nyuma kabisa kwenye hiyo nchi ya milima, kamwe hakuona garimoshi maishani mwake mwote.), bali nilimshika mikononi mwangu na kumwombea. Labda alikuwa na uzito wa ratili hamsini, amekauka tu. Na kwa hiyo, alikuwa maskini bikizee. Alikuwa amekokoka, naye akanikumbatia shingoni, na jambo la mwisho alilosema, “Mungu aubariki maskini moyo

wako sasa na hata milele.” Naye akaenda kuwa pamoja na Bwana. Na, huyo alikuwa ni mamake baba yangu.

²¹ Nami ninamkumbuka maskini mwanamke huyu, aliweka maskini ni—ninii yake, alikuwa na maskini aproni yake, angeivaa akienda kanisani, hakuishi mbali, nasi sote tulikuwa maskini. Basi akanyosha mkono chini ya huo mfuko, maskini mfuko huu mdogo, na kutoa moja ya hizo pochi ndogo za mfukoni ambazo hufungika kwa sauti, mwajua, akiingiza mkono humo atoe hizo nikeli. Loo, jamani! Ningalichukua hizo, ningejisikia kama Yuda aliyechukua pesa zile, vile vipande thelathini vya fedha.

²² Nami nikamwona akinyosha mkono, nikaangalia hilo, bongwe kubwa mno likaingia. Unajua jinsi hisia hiyo kwenye koo lako, kama uvimbe? Nikasema, “Loo, nilikuwa tu nikiwatania, sikumaanisha hilo.” Nikasema, “Nilitaka tu kuona kile mngesema.”

Huyu hapa shemasi kanisani, akiwa na hiyo kofia mkononi mwake, akaniangalia, na kusema, “Nifanyeje?”

²³ Nikasema, “Irudishe tu kofia yangu. Mbona, nilikuwa tu *nikiwatania*.” Mnaona? Nilijua kama angeweka hiyo nikeli au senti mle ndani, nisingeweza kuitumia. Kwa hiyo, kamwe sitasahau. Mpenzi, anajua habari zake. Nikasema . . .

²⁴ Nikaenda kule, nami nilikuwa na baiskeli kuukuu ambayo Ndugu John Ryan, kwa kweli alikuwa kwa namna fulani kama Nyumba ya Daudi, nywele ndefu, naye akaileta kule chini, na kunipa. Haikuwa—haikuwa imerudi nyuma, ilikuwa tu imechakaa, hivyo tu. Kwa hiyo, nikaenda kwenye duka la mali rahisi nikanunua mkebe wa rangi, kisha nikaipaka rangi, na kuiweka uwanjani, na kuiuza kwa dola tano, Haikunibidi kuchukua sadaka. Kwa hiyo, hapo ndipo nilikuwa karibu sana kuchukua sadaka.

²⁵ Kwa hiyo, hatuko hapa kwa kusudi hilo, tuko hapa kujaribu kuwasaidia, kujaribu kufanya jambo fulani ku—kuufanya, ujirani hapa rahisi kidogo kufanya mema, vigumu kidogo kufanya mabaya, kufanya maisha yapendeze zaidi kidogo kwenu, labda, kwamba Mungu ataponya magonjwa yenu na kurefusha siku zenu, kuokoa waliopotea, kuyasaidia makanisa. *Hawa* ndio wadhamini wangu, ni watu wanaoamini jambo lile lile ninaloamini, wasingekuwa wameketi hapa kama hawakuamini jambo hilo. Nao, kwangu mimi, ndio walio bora sana. Sasa, ni—ninamaanisha hilo, si kuwa . . .

²⁶ Baadhi yao hapo wakiwa na mvi, wenye umri mkubwa kuliko mimi, walikuwa huku nje wakihubiri pembeni kwa gi—gita na tari, nilipokuwa tu mvulana mwenye dhambi. Kwa hiyo ninajisikia duni kusimama mbele za watu hawa, alasiri ya leo, wanapaswa kuwa hapa. Waliifanya barabara kuwa rahisi kwangu kupitia, wakihubiri mambo haya yangekuja, nayo haya

hapa yanakuja. Kwa hiyo mmoja hupanda, mwingine hutia maji, Mungu hupata ongezeko, hivyo ndivyo itakavyokuwa.

²⁷ Na kwenye ile asubuhi kuu Kule, wakati meza itakapowekwa kwenye anga za mbingu, wakati maisha yote yamekwisha, tumeketi kwenye Karamu ile ya Arusi (ninataka kuwa huko sana, ndugu. Loo, ninatamani kuwa huko! Na—naamini nitakuwa huko, nikiishi vizuri na kujitahidi sana, Mungu ataniruhusu kuja kule, si kwa yale nifanyayo, bali kwa neema Yake.), nitanyosha mkono mezani na kupeana mikono na baadhi yenu nyote, niseme, “Ninakukumbuka, ulikuwa Yakima,” mnaona, “duniani.” Hapana shaka chozi dogo litatiririka mashavuni mwetu kwa furaha.

²⁸ Ndipo jambo kuu: Kumwona Mfalme akitoka, uzuri Wake wote, kuyapangusa machozi kutoka machoni mwetu, aseme, “Msilie, enyi watoto, yote yamekwisha sasa. Ingieni katika furaha ya Bwana, mliyowekewa tayari tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu.”

²⁹ Hilo ndilo ninalotaka kusikia, ndipo tutabadilishwa kutoka kwa kiumbe hiki tulicho, tuwe wasiopatikana na mauti, tumefananishwa na mwili Wake Mwenyewe wenye utukufu. Ndipo taabu za siku zenye joto, na kupepea, na kadhalika, zote zitakwisha basi, tutaingia katika amani ya Bwana milele. Mpaka wakati huo, hebu na tufanye kazi, tujitahidi, na kuomba, tukikutazamia Kuja kwa Bwana.

³⁰ Yohana Mtakatifu, mlango wa 14, na hebu tuanzie kwenye kifungu cha 7, na tusome kifungu cha 12 vyote pamoja. Yesu akinena:

Kama mngaliniuja mimi, mngalimjua na Baba yangu: na tangu sasa mnamjua, tena mmemwona.

Filipo akamwambia, Bwana, utuonyeshe Baba, yatutosha.

Yesu akamwambia, Mimi nimekuwapo... nanyi siku hizi zote, wewe usinijue, Filippo? aliyeniona mimi amemwona Baba; basi wewe wasemaje... , Utuonyeshe Baba?

Husadiki ya kwamba mimi ni ndani ya Baba, na Baba ndani yangu? hayo maneno niwaambiayo mimi, siyasemi kwa shauri langu, lakini Baba akaaye ndani yangu huzifanya hizo kazi.

Mnisadiki ya kwamba mimi ni ndani ya Baba... Baba yu ndani yangu: la, hamsadiki hivyo, sadikini kwa sababu ya kazi zenyewe.

Amin, amin, na—Amin, amin, nawaambieni, Yeye aniaminiye mimi, kazi nizifanyazo mimi, yeye naye atazifanya; na kubwa kuliko hizo atafanya; kwa kuwa mimi naenda kwa Baba.

31 Na somo langu la alasiri hii ni: *Tuonyeshe Baba Itatutosha*. “Kututosha” maana yake ni *kuridhisha*. “Kama utatuonyesha Baba, itaturidhisha.”

32 Sasa, nitachukua hili... Imekuwa ni shauku ya moyo wa mwanadamu tangu kumekuwako na binadamu, wanataka kujua, “Mungu yuko wapi? Laiti ningaliweza kumwona Mungu!”

33 Na sasa nitazungumza juu ya njia nne mbalimbali za kumwona Mungu. Na jana usiku, nilichukua somo la *Mabwana*, katika mlango wa 12 wa Yohana Mtakatifu, *Mabwana, Sisi Tunataka Kumwona Yesu*.

34 Nami naamini wote waliokuwa hapa jana usiku wakiwa na akili timamu, wakijua lolote kuhusu Maandiko, walimwona Yeye akitenda kazi miongoni mwa watu. Kama hukumwona, ninaamini karibu umepita matumaini, unaona, kama wewe—kama hukuliona. Baada ya Maandiko kuwekwa, imara tu, kote kuanzia Mwanzo na kuendelea kote katika Maandiko, yale hasa aliyoahidi hapa katika siku za mwisho, na hapa tumemwona akiingia jengoni jana usiku, kwa kuwa Mkristo huangalia yasiyoonekana. Mnajua hilo? Silaha zote za Kikristo hazionekani: upendo, furaha, amani, subira, wema, upole, utu wema, uvumilivu; matunda yote ya Roho hayaonekani.

35 Watu wanasema, “Nimetoka Missouri, kuona ni kuamini.”

36 Basi kamwe usingeweza kuwa Mkristo, maana inakubidi kumkubali Mungu kwa imani. Unaona? Huna budi kumwamini Yeye.

37 Na jana jioni, tulipomwona akiingia katika Roho, akasonga mbele na kuthibitisha ndani ya watu Wake, waaminio humu jengoni, waliendelea, na kumwona akifanya yale hasa aliyofanya alipokuwa hapa duniani, akithibitisha Maandiko, “Kazi nizifanyazo Mimi, ninyi nanyi mtazifanya,” na kuona matokeo yale yale kwa wanadamu waliojisalimisha kabisa kwa Mungu, mpaka Roho Mtakatifu aweze kutenda kazi kupitia kwa wanadamu hao kama tu vile Roho Mtakatifu alivyofanya kazi kupitia Yesu, Ambaye ndio kwanza akiri ya kwamba, “Mimi na Baba Yangu ni Mmoja. Baba Yangu anakaa ndani Yangu. Yeye hufanya hizo kazi. Si Maneno Yangu, ni Maneno Yake.” Mnaona? Alikuwa amejitolea sana kwa Mungu, kisha akafa na kulitakasa Kanisa kusudi apate kuishi ndani apate kuendeleza kazi Zake mpaka yale majilio ya kuja Kwake—Kwake mara ya pili, Yeye anakuja mara ya pili.

38 Sasa, tutaona kama tunaweza kumwona Mungu. Ni wangapi wangetaka kumwona Mungu? Hebu tuone mikono yenu. Na—najua ni utoto, bali tunapaswa kuwa watoto. Tunapofikia kujua mengi sana, basi hatujui lolote tunalopaswa kujua, Biblia ilisema. Daima hatutaki kupata hisia kubwa ya kiakili kwamba

tuko juu ya mtu fulani, ama kujua zaidi ya mtu mwingine, kuwa tu wa kawaida na rahisi.

³⁹ Watu hujaribu kumwelezea Mungu ndipo wanapitia juu yake moja kwa moja. Watu wanamtafuta Mungu *huko* nje kabisa, wakati Yeye amesimama papa *hapa*. Mnaona? Hiyo ni kusema, unaninii tu—wewe... Urahisi wake huwatatanisha tu watu mashuhuri wenye akili nyingi wanaojaribu kumfanya kitu fulani kikuu asicho. Yeye yuko hapa pamoja nasi, Yeye ni Mungu. Ninii tu, Yeye—Yeye ni sehemu yako, Yeye ni mshipa wako. Sisi ni mwili wa mwili Wake, na mfupa wa mfupa Wake, sisi ni sehemu Yake, maana sisi ni watoto Wake, naye Mungu anaishi ndani yetu, kama tu alivyofanya katika Mwanawe, Kristo Yesu.

⁴⁰ Sasa, tutamwangelia Mungu katika njia nne. Sasa, tatu ni thibitisho, bali tutatupa moja ya ziada humo alasiri ya leo, kulifanya dhahiri. Mtu yeyote anajua ya kwamba—ya kwamba wawili ni ushahidi, watatu ni thibitisho. Mimi... .

⁴¹ Wayahudi walimwambia Yesu, “Tunajua ya kwamba Wewe ni pepo, kwa sababu Wewe unajishuhudia Mwenyewe.”

⁴² Inahitaji wawili kushuhudia, Yesu alisema, “Mimi ni Mmoja, na Baba akaaye ndani Yangu ndiye Huyu mwingine. Kama hamwezi kuniamini Mimi, aminini kazi anazofanya ndani Yangu,” mnaona. Kwa hiyo hilo likafanya thibitisho la Wawili. Lakini sasa, tatu... .

⁴³ Na sasa, tutachukua njia nne za kumwona Mungu. Kwanza, “Mungu Katika Ulimwengu Wake,” “Mungu Katika Neno Lake,” “Mungu Katika Mwanawe,” “Mungu Katika Watu Wake.”

⁴⁴ “Mungu Katika Ulimwengu Wake,” tutaona kama tunaweza kumwona katika ulimwengu; “Mungu Katika Neno Lake,” tutaona kama tunaweza kumwona katika Neno; “Mungu Katika Mwanawe,” tutaona kama Yeye yuko ndani ya Mwanawe; halafu, “Mungu Katika Watu Wake,” tuone kama Yeye yuko ndani ya watu Wake. Hizo ni njia nne tunazoweza kumwona Mungu.

⁴⁵ Yule kafiri alisema, “Hebu nimwone.”

⁴⁶ Siku moja, nilikuwa nikizungumza kwenye kona, kulikuwa na kafiri ambaye alikuwa akizungumza kwenye kona ya pili. Naye alikuwa, alikuwa na Biblia imewekwa pale, kasema, “Ndicho kitabu kichafu sana, kiovu kuliko vyote kilichowahi kuandikwa.”

⁴⁷ Na, loo, alikuwa tu akiendelea. Alikuwa, alikuwa kasisi, ama, alisomea ukasisi katika nyumba ya watawa, na ni mwanatheolojia kwelikweli, alilijua Neno. Na kwa hiyo, alikuwa akitafuna tumbaku. Naye, nilikuwa nimesimama karibu na duka dogo la vyakula, basi wakati alipokuja kununua vyakula, basi hapa mhubiri na kafiri wakakutana pamoja. Kwa hiyo, akasema, “Loo, wewe ndiye yule mhubiri anayepiga makelele hapa chini.”

Kasema, “Naam, bwana, mimi ndiye.”

Naye akasema, “Huamini upuuzi huo unaosema.”

Nikasema, “Kwa moyo wangu wote, ninauamini.”

⁴⁸ Nami nilijua alikuwa mwerevu kuwa katika nyumba ya watawa, mnaona. Kwa hiyo, nikasema, “Naam, bwana, ni—ninauamini kwa moyo wangu wote.” Kwa hiyo, nilijua alinizidi sana kiakili, lakini nilijua nilikuwa na Mungu ambaye angeweza kushinda chochote ambacho ibilisi angeweza kuleta, kwa hiyo nilishikilia tu, nione kile Mungu angesema.

Akasema, “Kama nitakuthibitishia hakuna jambo moja katika yale unayonena, je, utalikubali?”

Nikasema, “Siamini ungeweza kufanya hivyo.”

Akasema, “Hakuna kitu kama Mungu.”

Nikasema, “Hayo ni maoni yako, maoni yangu ni tofauti.”

Naye akasema, “Vema, angalia, mwili wa mwanadamu una hisi ngapi?”

Nami nikasema, “Vema, ina hisi.”

“Ulienda shule umbali gani?”

Nikasema, “Mbali vya kutosha kujua kuna Mungu.”

Na—naye akasema—akasema, “Vema, taja hisi za binadamu.”

Nami nikasema, “Kuona, kuonja, kugusa, kunusa, na kusikia.”

⁴⁹ Akasema, “Sasa, kama Yeye ni Mungu wa mwanadamu, kwa mwanadamu, hakika moja ya hizo hisi ingemtangaza.” Akasema, “Sasa, uliwahi kumwona? Uliwahi kumwonja, kumnusa, kumgusa, ama kumsikia?”

Nikasema, “Nilimgusa; ninamgusa sasa.”

Akasema, “Hebu nimguse.” Hisi hiyo ya kugusa huenda vivyo hivyo, unaona, kwa vidole vyako.

Na—nami nikasema, “Vema, inawezekana kwamba ningeweza kumgusa, wala wewe usingeweza kumgusa.”

Akasema, “Loo, la, la, huwezi kuivuta saikolojia yako juu yangu.”

⁵⁰ Ndipo nikachukua pini na kumdunga. Naye akasema... Nilifikiri atanipiga kofi kwanza, lakini nikarudi nyuma asinifikie. Ndipo nikasema, “Nilifanya hivyo kwa kusudi fulani, bwana, samahani, bali ninataka tu kutoa hoja.” Nikasema, “Ulihisi huo?”

Akasema, “Bila shaka niliuhisi.”

Nami nikasema, “Lakini sikuuhisi.”

Akasema, “Hebu nikudunge.”

Nami nikasema, “Naam, wewe amini jambo lile lile ninaloamini, nawe utapata matokeo yale yale.” Hiyo ni kweli.

⁵¹ Inawezekana ungeweza kuwa na mkamba tumboni mwako, nami nisingejua lolote kuuhusu, bali ni halisi kwako. Unaona? Lakini haingekuwa kwangu mimi, isipokuwa nilikuwa na mkamba ule ule tumboni mwangu, ama kuumwa na kichwa, ama chochote kile.

⁵² Kwa hiyo basi, nikasema, “Vema...” Nami nilikuwa nifikiria...Naye alikuwa, unajua una...Mama alizoea kusema, “Ukimpa ng’ombe kamba ya kutosha, atajinyonga.” Kwa hiyo hivyo ndivyo wewe...Ni—niliichezea saikolojia yake. Nami nikasema, “Unajua nini? Wewe ni mtu mwerevu sana.”

Akasema, “Mama yangu kamwe hakulea wapumbavu wowote.”

Nami nikasema, “Vema, hilo ni jambo zuri.”

⁵³ Nikasema, “Hakika nisinge—nisingejua,” Nisingeweza kusema, “kwa sababu Biblia ilisema, ‘Mpumbavu alisema moyoni mwake hakuna Mungu.’” Mwajua, lakini ni—nisingeweza kusema hilo papo hapo, maana nilikuwa nikimwelekeza moja kwa moja kufikia mahali nilipomtaka.

Ndipo nikasema, “Una moja ya akili hodari sana nilizowahi kuona, uh, niliyewahi kuzungumza naye, mtu aliyekuwa na akili timamu kama wewe.”

Akasema, “Hiyo ni kweli.”

⁵⁴ Loo, alijaa majivuno. Hapo ndipo nilijua ilinibidi kumchezea, ilikuwa ni papo hapo. Nami nikasema, “Utakubali ya kwamba una akili?”

Naye akasema, “Mbona, hakika! Kwa nini? Unajifanya kana kwamba umepoteza yako.”

Nami nikasema, “La, sidhani nimepoteza.” Lakini nikasema, “Nashangaa tu kama kweli una akili.”

Naye akasema, “Unasema nini?”

Nikasema, “Ni akili ya binadamu, sivyo?” Yeye akashika papo hapo kile nilichokuwa nikitaka kufanya.

Akasema, “Sasa, ninii tu...”

Nikasema, “La, bwana, nilikuwa muungwana, nilijibu ninii lako...” Nikasema, “Taja hisi za mwili.”

“Vema,” akasema, “unazijua.

Nikasema, “Nataka uzitaje.” Nikasema, “Nilikutajia nilipokwambia nilizijua.”

Akasema, “Kuona, kuonja, kugusa, kunusa, na kusikia.”

Nikasema, “Je, umewahi kuona akili yako? Uliwahi kuinusa, kuionja, kuisikia?”

“La.”

Nikasema, “Basi huna akili.”

Akasema, “Loo, najua nina akili.”

Nikasema, “Ninajua nina Mungu, pia, bwana.” Nikasema, “Ni—ninajua tu hilo.”

⁵⁵ Kwa hiyo, silaha zote za Mungu hazionekani, bali Mkristo huangalia yasiyoonekana, kama vile Ibrahimu alivyoviita vitu ambavyo havikuwako kana kwamba vilikuwapo kwa sababu Mungu alikuwa amesema hivyo. Kwa hiyo tutaangalia sasa, si kwa yasiyoonekana, alasiri ya leo, bali njia nne ambazo tutaninii, tungeweza kuchukua dazani moja, bali tutachukua tu njia hizo nne kwa ajili ya thi—thibitisho ya kwamba Mungu yu hai sasa hivi. Mungu yupo papa hapa alasiri ya leo, papa hapa katika chumba hiki. Yeye aliahidi, “Walipo wawili watatu wamekusanyika katika Jina Langu, nitakuwa katikati yao.”

⁵⁶ Sasa, tutazungumza kwanza juu ya “Mungu Katika Ulimwengu Wake.” Sasa, dunia ingeweza kujishikilia katika anga iliyomo? Hata hivyo, upande wake wa juu na wa chini ni upi? Ni nani ajuaye? Wale walio huko chini Kaskazini... kwenye Ncha ya Kusini wanajisikia tu kama wako juu, sawasawa na wale walio kwenye Ncha ya Kaskazini. Kwa hiyo mnaona, ni ninii tu, wanasukuma upande *huu*, ambao ni kusukuma chini, tunafikiri tuna—wanaelekeza juu. Mnaona? Wanafikiri wanaelekeza juu, wakati kwetu wanaelekeza chini. Tunapoelekeza juu, mbona tunaelekeza chini kwao.

⁵⁷ Kwa hiyo, inaning’inia hewani. Ni kitu gani kinachoishikilia huko? Hebu tupa mpira mle ndani na kuuzungusha upesi utakavyo, dunia hii inazunguka zaidi kidogo ya maili elfu moja kwa saa, maili elfu ishirini na tano kuizunguka, inazunguka, inafanya mzunguko mkamilifu kila saa ishirini na nne, lakini kwa hiyo, inafanya bora kidogo kuliko maili elfu moja kwa saa inapozunguka, vema, hebu zungusha mpira hewani, na, vile vile kwa mwendo ule ule, unaona, haungefanya mzunguko mmoja katika duara ile ile, ungeanguka. Ama ingekuwa ni kupanda juu, kushuka chini, kwenda kando, ama kitu fulani.

⁵⁸ Ni kitu gani kinachoishikilia kule? Tunajua imekuwa hapa kwa miaka elfu sita, tuna kumbukumbu yake, kwamba imesimama hapa mahali pale pale. Nao wanaweza kuipimia muda kwa mwezi na nyota kikamilifu sana, hata haitakosa sekunde moja, wanaweza kubashiri miaka ishirini mbele wakati kupatwa kwa jua kutakapotokea, wakati mwezi na jua vitakapopita.

⁵⁹ Kila kitu hufanya kazi kwa upatanifu kwa Mungu, viumbe vyote vya Mungu, ila mwanadamu. Kwa hiyo, mwanadamu ni mwanawe, anayejisikia kwamba anajua kidogo tu zaidi ya Baba ajuavyo, kwa hiyo, tunajaribu kuwazia yote, badala ya kuamini tu yale aliyosema kulihusu, hivyo tu.

⁶⁰ Siku moja, kafiri mmoja aliniambia, akizungumza juu ya mwezi wote na jua, na jinsi lilivyomemetesha kipande kidogo kikaanguka.

⁶¹ Nikasema, “Utathibitishaje hilo?” Nami nikasema, “Jambo pekee unaloweza kufanya ni kulithibitisha kwa imani.” Kisha nikasema, “Ninataka kukwambia sasa, imani yangu ni dhaifu sana kwa hilo. Ninaamini tu yale Biblia iliyosema, Hilo ndilo jambo pekee ninaloamini, ni yale Mungu aliyosema. Yeye aliumba Mbingu na nchi, nami ninaamini tu hivyo. Kwa hiyo hiyo ndiyo imani niliyo nayo, ni yale Mungu aliyosema kulihusu.”

⁶² Na sasa, basi ingewezekanaje kamwe? Ua hilo dogo lingewezaje kuishi, alasiri ya leo, mzabibu huo, lingewezaje kuishi, mmea, hasa, bila Mungu? Wanasayansi wote ulimwenguni wasingeweza kutengeneza moja ya majani hayo hapo. Wanaweza kuunda kitu kinachofanana nalo, bali wasingeweza kuunda jani hilo, kwa sababu jani hilo lina uhai ndani yake, na sayansi kamwe haiwezi kuzalisha uhai.

⁶³ Ua dogo, ukichukua, kama ninyi wanawake hapa, inakuwa baridi hapa bondeni, ninazunguka, ninaona bustani zenu za maua sasa, nilikuwa nikiendesha huku na huko muda mfupi uliopita, nikijaribu kuweka akili yangu juu ya Mungu, na kuomba, “Bwana, fanya jambo fulani hapa bondeni, tafadhali, wasaidie watu Wako, ni saa yenye giza sana,” huku nikipanda na kushuka barabarani, nikiomba, ndipo nikapita na kuona hayo maua ya kupendeza. Sasa, haitachukua muda mrefu mpaka jalidi italipiga maskini ua hilo, litainamisha maskini kichwa chake life, baadhi yake yatakuwa machanga, yenye umri wa makamu, na ya siku nyingi, kutoka hapo linadondosha mbegu ndogo nyeusi.

⁶⁴ Amini usiamini, Mungu ana msafara wa mazishi kwa ajili ya maua Yake. Mlijua hilo? Hakika anao, mvua ya masika inakuja na kulia machozi makubwa mno kutoka angani, na kuizika maskini mbegu hiyo nyeusi chini ya ardhi. Hiyo ni kweli kabisa. Majira ya baridi kali yanakuja na kuigandisha hiyo mbegu, inapasuka, nyama inatoka, na sasa, inagandia huko chini inchi kadhaa, ubua imekwisha, balbu imekwisha, petali imekwisha, mbegu imekwisha, nyama yake imekwisha. Je, huo ndio mwisho wa hilo ua? La, bwana. Mara tu ju—jua linapochomoza mashariki na joto linaanza, sasa, huwezi kuchukua taa na kuliangazia, na kulifanya, inahitaji nuru ya jua, kuweka nuru ya jua juu yake na kuanza kulipasha joto, litafufuka tena.

⁶⁵ Mungu aliificha hiyo chembe ndogo zazi mahali fulani kusudi ipate kuishi tena, kwa sababu iko katika—katika mapenzi ya Mungu. Ni mmea wa Mungu, Mungu aliuweka hapa kwa kusudi fulani, nao haugombani wala kuwa na hamaki,

unatumikia tu kusudi ambalo Mungu aliuweka hapa kwa ajili yake.

⁶⁶ Na laiti tungefanya tu hivyo, tutumikie kusudi ambalo Mungu alituweka hapa kwa ajili yake! Sio tu kuwa, hatuna budi kufuga nguruwe, na hilo ni sawa, hatuna budi kufanya *hivi, vile*, ama *vinginevyo*, bali Yeye alituweka hapa tuwe wana na binti za Mungu kumtukuza Yeye, na kumsifu kama lile ua dogo.

⁶⁷ Nilihubiri juu ya somo si muda mrefu uliopita *Tazama Mayungiyungi*, nami nikachukua yungiyungi, Mchungaji Yungiyungi, jinsi anavyoufungua moyo wake, nyuki hutoa sehemu yake, nao watalii wanapita, “*kunusa*,” harufu hiyo nzuri, kila kitu kinapata sehemu ya Bw. Yungiyungi, naye hana budi kujitahidi usiku na mchana kuizalisha hiyo. Hivi hamwamini Mungu yuko katika ulimwengu Wake? Kila mahali, Mungu yuko.

⁶⁸ Huko nyumbani kwangu, ninaishi kwenye Mto Ohio, na loo, nayapenda maji sana, basi kulikuwa na mvulana mdogo aliyeishi huko chini mjini, naye akaenda kanisani, na alikuwa ni mvulana mdogo, mzuri. Ndipo akamwambia mama yake siku moja, akasema, “Mama, nataka kukuuliza swali.” Kasema, “Ninamsikia mhubiri akinena kuhusu Mungu kwamba ni mkuu sana.” Kisha kasema, “Sasa, nashangaa tu kama mtu yeyote angeweza kumwona Mungu?”

“Mbona,” akasema, “Mpenzi, mwulize mwalimu wako wa shule ya Jumapili.” Kasema, “Mama asingeweza kujibu hilo, sijui lolote kulihusu.”

Na kwa hiyo wakamwuliza mwalimu wa shule ya Jumapili, naye akasema, “Loo, nisingejua kuhusu hilo. Unapaswa kumwuliza mchungaji.”

Kwa hiyo akaenda na kumwuliza mchungaji, naye mchungaji akasema, “La, mwanangu, hakuna mtu anayeweza kumwona Mungu. Hakuna mtu anayeweza kumwona Mungu na kuishi, kamwe huwezi kufanya hivyo.”

⁶⁹ Kwa hiyo maskini jamaa huyo alivunjika moyo. Alishirikiana na mzee mvuvi aliyeishi mtoni. Basi siku moja, walikuwa huko karibu na [Ndugu Branham anakohoa—Mh.] (Samahani.) Kisiwa cha Naili Sita, ndipo dhoruba ikatokea. [Ndugu Branham anasafisha koo lake.] (Samahani.) Ndipo kukatokea dhoruba, nayo maji, mnajua jinsi yanavyoingia baada ya mvua, majani yote yamechukuliwa na maji.

⁷⁰ Maskini huyo mvuvi akarudi ndani ya mtumbwi, akaanza kuteremka mtoni akivuta mtumbwi wake. Na kama tu vile mvuta makasia, ama baharia yeyote ajuavyo, uwiano wa ncha hiyo ya wimbi kwenye makasia, namna *hiyo*, alipokuwa akishuka, alikuwa akivuta sanduku la samaki nyuma. Na kulikuwa na, jua lilichomoza magharibi, upande *huu*, na alikuwa akiangalia upande wa mashariki, yule mvuvi mzee alikuwa,

ndipo upinde wa mvua ukatokea angani. Basi maskini jamaa huyo alikuwa ameketi kwenye shetri ya mashua, na kwa hiyo akaanza kumwona yule mvuvi mzee na ndevu zake zenye mvi, machozi yakaanza kutiririka mashavuni mwake alipoutazama ule upinde wa mvua, akienda mbele.

⁷¹ Ndipo maskini jamaa huyo akashikwa na shauku, naye akakimbia hadi katikati ya mashua, akamshika huyo mzee mvuvi magotini na kuanguka pale miguuni pake, akasema, “Bwana, nitakuuliza swali mwalimu wangu wa shule ya Jumapili, mama yangu, mchungaji wangu, hakuna mtu angaliweza kujibu: Je, mtu yeyote angeweza kumwona Mungu?”

⁷² Ndipo yule mvuvi mzee asingeweza kujizuia, akavuta tu makasia kwenye mashua, akamkumbatia huyo mvulana mdogo, akasema, “Mungu aubariki maskini moyo wako, kipenzi. Yote niliyoona kwa miaka hamsini iliyopita imekuwa ni Mungu.” Kulikuwa na Mungu mwingi sana ndani yake, kila kitu alichoaangalia kilikuwa ni Mungu.

⁷³ Hivyo ndivyo unavyomwona Mungu ni wakati unapomwingiza Mungu ndani yako. Unamwacha Yeye aangalie kupitia macho yako, hivyo ndivyo utakavyomfanyia Mungu kazi, wakati Mungu anapoweza kutumia mikono yako, kutumia miguu yako, kutumia midomo yako, kutumia ulimi wako, kutumia masikio yako, kutumia macho yako. Mungu, ndani yako, humwona Mungu kwa nje. Mungu yuko katika ulimwengu Wake. Alikuwa kwenye upinde wa mvua, akatatua swali pale ambalo hakuna mmoja wao angeweza kulitatua.

⁷⁴ Mimi ni mwindaji, kama nyote mjuavyo. Mama yangu ni nusu-Mhindi, na mimi, wala wongofu wangu kamwe haukuondoa hilo kutoka kwangu, ningali ninaenda huko Colorado ambako mimi ni kiongozi mwenye leseni, na kila msimu wa kupukutika majani, na kupanda juu sana milimani ambako nilikuwa nikichunga ng’ombe kwa miaka mingi, na kuketi pale mara nyingi, nikajifunza mengi sana kumhusu Mungu. Ninakumbuka nikiketi pale, nimeuweka mguu wangu kukingama... ambapo Shirika la Hereford huwalisha kwenye Bo—Bonde la Mto Troublesome, na kuwaangalia wafugaji tunapowaingiza ng’ombe humo ndani, tukiwaweka kwenye majira ya kuchipua wapate kuchungwa.

⁷⁵ Na hili hapa jambo moja mimi, sababu ya mimi kuwa asiye na mipaka ya kimadhehebu. Mlinzi alisimama pale kwenye ua unaohama, naye akawaangalia hao ng’ombe. Kama unaweza kuchangia tani moja ya nyasi kavu kwenye ranchi yako, ukichangia tani nyingi za nyasi kavu, unaweza kuweka ng’ombe msituni; nadhani mngali mna sheria zizo hizo hapa. Na halafu, yule mfugaji akisimama pale akiwakagua hao mifugo, hakujali sana ni chapa gani walizobandikwa.

⁷⁶ Yetu ilikuwa Tripod, na hao wengine, jina lililokuwa juu yetu lilikuwa Turkey Track, na hapo juu kidogo tu kulikuwa na Grimes, hilo shirika kubwa lililokuwa na Bar, Diamond Bar, na wengi wa ninii, baadhi yao waliweka mamia na mamia ya ng'ombe mle. Lakini mnajua, huyo—huyo mlinzi kamwe hakujishughulisha na hizo chapa, alichunguza kibandiko cha damu kwenye sikio. Usingeweza kumweka Hereford kwenye msitu huo bila, ama, ng'ombe kwenye msitu huo ispokuwa awe ni Hereford ukoo safi, ilibidi awe ni Hereford aliyesajiliwa.

⁷⁷ Nami nafikiri kwenye ile Siku ya Hukumu Mungu hataangalia kama mimi ni mfuasi wa Assemblies, ama Church of God, ama ni kanisa gani ninaloshiriki, chapa nivaayo, ataangalia kibandiko cha Damu, Damu ya Mwanawe Mwenyewe, hicho ndicho Yeye ata—atakachoangalia. Hakuna kitu kitakachoingia mle ila Mkristo aliyezaliwa mara ya pili.

⁷⁸ Tuliwinda kulungu, kulungu huko juu sana mwaka huu, kwa sababu hakukuwako na theluji ya kuwafanya washuke chini. Naye Bw. Jeverez, ambaye alikuwa mmoja wa wamiliki wa moja ya hizo ranchi, tulijua kila sehemu ya ardhi katika nchi hiyo ya msitu kule kwa maili mia moja, maana tulikuwa, kwa kuwa niliwachunga ng'ombe, na kuwapa chumvi, na kadhalika, kapanda magari-moshi ya mizigo, na kurudi, na kuwapa ng'ombe chumvi, na kuwakusanya, na kadhalika.

⁷⁹ Nasi tulikuwa tumeenda kuwinda, naye ni mwindaji mzuri sana, naye alikuwa ameelekea upande wa kushoto kurudi kwenye, kile tunachokiita, West Fork, nilielekea East Fork. Nasi tungekutana katika siku nne au tano, na kuwaanika kulungu wetu, na chochote tulichokuwa tunaenda kupata, na kisha kuwaweka farasi wetu pamoja, na kuchukua mizigo na kuja, kuwaletemsha chini. Nilikuwa huko juu sana, nikitembea huko juu, na hakukuwa—hakukuwako na theluji ya maana. Na—na katika majira ya kupukutika majani ya mwaka, huko juu milimani, kutakuwa na theluji, kisha mvua, na ndipo jua litawaka. Mnajua jinsi ilivyo, kubadilika kwa hali ya anga mnamo Oktoba.

⁸⁰ Nami nilikuwa nikitembea juu sana, karibu sana na mpaka wa msitu, ndipo ikatokea dho—dho—dhoruba ya Kaskazini, nazo mbingu zikageuka kijani kibichi kwa kitambo kidogo, na loo, ikaanza kuvuma, na kunyesha, huku—huku mvua ya theluji ikinyesha. Nami nikaenda nyuma ya mti, na kusimama tu nyuma ya mti, nikailaza bunduki yangu chini, kulikuwa na uwazi wa siku nyingi hapo karibu, basi nikailaza bunduki yangu pale chini, nami nilikuwa tu nikiwazia, “Ee, Mungu, jinsi Wewe ulivyo mkuu! Jinsi Wewe ulivyo wa ajabu! Wewe ni ninii sana . . .

“Uliumba milima,
Ulibubujisha chemchemi,
Ukainua mlima,

Bwana weka mikono Yako ya thamani juu yangu.”

⁸¹ Nilipokuwa nimesimama pale nikingojea mvua inyeshe, ndipo upepo ukawa mkali sana, basi baada ya dhoruba kwisha, nikamsikia kulungu dume akianza kulia, alikuwa amepotea katika hiyo dhoruba. Huko juu kabisa kando ya kilima, mbwa mwitu akapiga mayowe, mwenzake akajibu huko chini kidogo. Mnajua wakati Daudi aliposema, “Kilindi huita kilindi,” kulikuwa na kitu fulani juu yake kilichokuwa cha kiungu kwangu, kusikia wito wa wanyamapori; huyo hapo yule kulungu.

⁸² Nikageuka na kuangalia nyuma kuelekea magharibi, kuelekea hapa Washington. Na mahali ambapo jua lilikuwa likishuka, likitua kupitia kwenye mianya ya milima, ilionekana kama jicho kubwa likiangalia, nikawazia, “Hiyo ni kweli, ‘Macho Yake yanaenda huku na huko juu ya nchi.’” Kila mahali ulipoangalia palikuwa ni Mungu, utauwa tu.

⁸³ Ndipo basi nikaangalia nyuma *hivi*, na kulikuwa na upinde wa mvua nyuma upande *huu*, juu ya, ambapo mimea isiyokauka ilikuwa imeganda kabisa kutokana na mvua, nayo ikafanyiza jua dhidi yake, ikafanya upinde wa mvua kuvuka hilo bonde. Mbwa mwitu akipiga kelele, kulungu wakipiga kelele, huku jua linatua, loo, jamani, nilisimama pale nikilia kama mtoto mchanga. Nikaangalia nyuma, nikasema, “Naam, kuna nini kwenye upinde wa mvua? Ni agano, ahadi.”

⁸⁴ Ufunuo 1, “Alionekana mithili ya jiwe la yaspi na akiki,” hao ni Benyamini na Reubeni, wa kwanza na wa mwisho; Yeye aliyekuwako, aliyeko, na atakayekuja; Shina na Mzao wa Daudi; Nyota ya asubuhi. Yote aliyokuwa, vyeo Vyake, Huyo hapo katika upinde wa mvua ameketi hapo, nami nikawazia, “Loo, jinsi inavyopendeza! Jinsi ilivyo vizuri kuwa hapa!”

⁸⁵ Nami nikafurahi sana, hata nikazunguka, nikauzunguka mti huo, kwa nguvu tu nilivyoweza, nikipiga mayowe kwa sauti yangu yote, yapata maili thelathini na tano kutoka kwa mwanadamu, nami nilikuwa tu nikipiga mayowe, na kupaza sauti. Nadhani kama mtu angekuja mwituni, wangedhani ya kwamba mtu fulani alitoka kwenye hospitali ya wendawazimu huko juu. Nilikuwa tu nikipiga mayowe na kupiga makelele, sikujali, nilikuwa nikimwabudu Mungu, nilikuwa tu nikijifurahisha.

⁸⁶ Nami ningesimama, nami ningewazia, “Hiyo ni kweli, Yeye ni Alfa na Omega, yeye yule jana, leo, na hata milele.” Na kuzunguka, na kuzunguka, na kuuzunguka huo mti tena, kwa nguvu tu niendavyo. Ilinibidi tu, ilinibidi kutoa baadhi ya hisia, mwajua, ilikuwa ninii tu, *kitu fulani* kilikuwa kikichemka, nami nikalia tu kwa sauti yangu yote.

⁸⁷ Ndipo baada ya kitambo kidogo, nikamsikia kuchakulo mdogo wa misonobari, sijui kama ninyi ndugu mnajua kile

walicho au hamjui, yeye ni polisi wa koti la samawati wa mwituni, akaruka juu ya kisiki pale, “*Chwi, chwi, chwi! Chwi, chwi, chwi!*”

⁸⁸ Nikawaza, “Loo, umesisimkwa na nini sana jamaa mdogo? Ninamwabudu Mungu aliyekuumba.” Nami nikazunguka na kuzunguka ule mti tena, kwa nguvu nilivyoweza. Nami nikawazia, “Vema, ninamwabudu Mungu yeye yule aliyekuumba. Yeye ni Muumba wangu, ninampenda, ninaabudu.” Nami nikaendelea kuuzunguka huo mti. Baada ya kitambo kidogo, nikasema, “Hivi hupendi hilo? Unapaswa kufanya hivyo mwenyewe. Wewe ni kiumbe cha Mungu, unapaswa kumwabudu Yeye, wewe mwenyewe.”

⁸⁹ Nikaja kugundua, yeye hakuwa akiniangalia, angekiinamisha maskini kichwa chake kwa upande, na kuangalia chini katika uwazi huo. Basi upepo ulikuwa umempeperusha maskini tai mle ndani.

⁹⁰ Sasa, tai ni mmoja wa ndege ninaowapenda sana, kwa hiyo, Mungu huwafananisha manabii Wake na tai. Yeye—Yeye anasema Mwenyewe, Yeye—Yeye ni Mwenyewe ni tai, Yehova-Tai. Labda, Bwana akipenda, ningetaka kuwahubiria juu ya jambo hilo wakati mmoja, *Kama Tai Ataharikishavyo Kiota Chake*.

Halafu basi, kwa hiyo wakati alipokuwa akiangalia upande namna *hiyo*, alikuwa akimwangalia tai huyu kule chini.

Ndipo tai huyu mkubwa akaruka huko nje, macho yake makubwa ya kijivu, nami nikawazia, “Loo, huyo ndiye aliyekusisimua. Um-hum.”

⁹¹ Vema, nikaanza kuchunguza jambo hilo, nami nikawazia, “Bwana, ninajua Wewe uko kwenye mlio huo wa kulungu huyo, uko kwenye mwito wa yule mbwa mwitu, uko kwenye upinde wa mvua, uko kwenye kutua kwa jua, uko ndani yangu, uko tu kila mahali, uko katika maua yote, Wewe—Wewe uko tu kila mahali, sasa, ungewezaje kunizuia kukuabudu Wewe, kuniruhusu nimwone maskini tai yule amesimama pale? Sasa, hakuna kitu kumhusu, yeye ni mnyang’anyi. Vema, vipi kuhusu yeye?” Nikasema, “Ulimleta kwa sababu gani? Ni nini...? Ninamwona Mungu huko nje, bali siwezi kumwona Mungu katika maskini tai yule.”

⁹² Vema, ikatokea nikaona pale, nikasema, “Aisee, jamani, unajua ningeweza kukupiga risasi?” Sasa, alijua nilikuwa ninavutiwa naye, napenda ushujaa wake. Alikuwa akiangalia... nilimwona... “Kwa nini huniogopi?” Nami nilimwona akichukua mabawa yake, mwajua, manyoya yake na kuyajaribu namna *hiyo*. Akaninii tu. . .

⁹³ Nikawaza, “Loo, kumbe, kumbe, Bwana.” Unaona? “Haogopi, ana mabawa mawili aliyopewa na Mungu. Anajua kabla sijagusa hiyo bunduki, angeweza kuingia kwenye msitu

ule pale, wala nisingemwona tena.” Mnaona? Nami nikawazia, “Kama angeweza, kama huyo tai, kwa kipawa alichopewa na Mungu cha mabawa mawili, kumwondoa kwenye—kwenye hatari, ni zaidi sana vipi Kanisa linapaswa, wakati wanapoweza kuhisi nguvu za Roho Mtakatifu karibu nao, tunapaswa kufanya nini? Tuweze kuruka tuondoke, kwa imani, kutoka kwa kila maradhi, kila ugonjwa, na kila kitu cha ulimwengu, kama tunaweza kuhisi Uwepo wa Mungu.”

⁹⁴ Mradi hayo manyoya yalikuwa yakienda vizuri, alijua angeweza kufanya hivyo, kwa sababu alikuwa na imani katika kipawa ambacho Mungu alikuwa amempa. Na hata hivyo, tunaketi na kushangaa na kuteka nyara, tukiwa na nguvu zenyewe za Roho Mtakatifu juu yetu, na kutembea. . . tukipitia jengoni tukionyesha ya kwamba Yeye yupo.

⁹⁵ Mbona, unamwona Mungu popote unapoangalia. Hivi huamini hilo? Mungu yuko katika tai, Mungu yuko katika mlio wa mbwa mwitu, Mungu yuko katika machweo ya jua, Mungu yuko katika ulimwengu Wake, Mungu yuko katika ua Lake, mbona, Mungu yuko kila mahali kama utaangalia tu kote.

⁹⁶ Kumalizia hadithi hiyo, maskini tai huyo, nilimwangalia kidogo. Basi maskini—maskini kuchakulo huyu mdogo wa misonobari amesimama pale, akiniangalia, mwajua, “*Chwi, chwi!*” akimwangalia yule tai. Basi baada ya kitambo kidogo yule tai akatosheka nayo, kwa hiyo akafanya tu mruko mmoja mkubwa, akapigapiga mabawa yake karibu mara mbili, huyo ametoweka.

⁹⁷ Sasa, nilimwangalia, hakusogeza ninii wake, unyoya baada ya hapo, alipofika juu ya msitu huo wa kijani kibichi, aliweka tu mabawa yake, alijua jinsi ya kufanya hivyo, ndipo wakati upepo huo, ukipanda mlimani, kila wakati upepo ungeingia, *whiu*, angepanda tu juu yake, apande juu yake. Nikasimama na kumwangalia, loo, jamani, alizidi tu kuwa mdogo zaidi na zaidi, mpaka akatoweka kabisa.

Ndipo nikawaza, “Jambo ndilo hilo. Jambo ndilo hilo, Bwana.”

⁹⁸ Unaona, sio, wakati ukiwa mgonjwa au mhitaji, si: *Papatika*, *papatika* kwa *hili*, “Peleka barua yako kwa kanisa *hili*, na Assemblies wasipokutendea mema, nenda kwenye Church of God, wasipokutendea mema, rudi kwa Baptisti.”

⁹⁹ Hilo silo. Ni kujua tu jinsi ya kuweka mabawa yako ya imani katika nguvu za Mungu, uondoke kwake, usonge mbele. Wakati Roho Mtakatifu anapoanza kutenda kazi, panda tu juu Yake.

¹⁰⁰ Si: *Papatika, papatika, papatika, papatika, papatika, papatika*, “Vema, nitaenda *huku* kama hamtanitendea mema. Nitarudi *hapa*. Nitapitia kwenye mstari wa maombi wa Roberts. Ndugu Branham anakuja, nitapitia wake.”

101 Hilo silo. Weka imani yako katika nguvu za Mungu kisha uondoke.

102 Alimwacha maskini huyo kindi, ama kuchakulo, ameketi pale akisema, “*Chwi, chwi, chwi!* Siku za miujiza zimepita. Hakuna kitu kama Uponyaji wa Kiungu. Hakuna ubatizo wa Roho Mtakatifu.” Aliiondokea tu.

103 Loo jamani! Hilo ndilo tunalotaka kufanya, kuinuka juu yake. Kuachana na hao watu wanaosema, “Hakuna kitu kama Uponyaji wa Kiungu. Mungu hatimizi Neno Lake. Yesu Kristo si yeye yule jana, leo, na hata milele.” Weka tu mbawa zako katika nguvu za Mungu na uondoke. Hiyo ni kweli. Wanaenda mahali wasipoonekana, waache wameketi peke yao. Iweni tu viziwi hata hamyasikii hata kidogo, yaondokeni tu. Mungu yuko katika ulimwengu Wake. Mungu hutenda kazi miongoni mwa viumbe Vyake.

104 Hebu mchukue maskini bata, mimi huenda kwenye misitu ya kaskazini wakati mwingine kuwinda, nimewinda kote ulimwenguni, nimeenda kwenye misitu ya kaskazini, kuna maskini bata mdogo aliyezaliwa huko juu kwenye ziwa hilo. Kamwe hakutoka kwenye ziwa hilo, alizaliwa mle kwenye majira ya kuchipua, lakini *kwa namna fulani*, wakati vilele vyenye theluji vinapoifunika milima na upepo huo mdogo baridi wa kwanza unashuka kupitia mlimani, kuna maskini bata fulani kwenye kidimbwi hicho, yeye ni maskini bata dume, anaenda moja kwa moja hapo nje katikati ya kidimbwi hicho, anachomoza maskini mdomo huo hewani, na kufanya, “*Honk, honk,*” na kila bata kidimbwini atamjia. Naam, bwana.

105 Atafanya nini? Atainuka kutoka kwenye hicho, mnakumbuka kamwe hajawahi kuwa nje ya kidimbwi hicho, bali atatoka moja kwa moja kwenye kidimbwi hicho na kuongoza kila mmoja wa hao mabata moja kwa moja hadi Louisiana kwenye mashamba ya mpunga awezavyo kwenda. Asipofanya hivyo, yote yatakuwa yameganda.

106 Hakika, tunapaswa kuwa na hisi ya bata. Kama Mungu anaweza kutumia silika ya bata kuwaongoza watu wake, ama, marafiki zake mabata waondokee mahali ambapo pangeganda, hakika nguvu za Roho Mtakatifu zinapaswa kutuongoza kwa Kristo ambaye ni Mponyaji wetu, na mbali na hatari. Mungu alikupa silika ya bata, alikupa Roho Mtakatifu. Loo, ninajisikia kubarikiwa sasa hivi! Naam, ninajisikia. Naam, Yeye alitupa Roho Mtakatifu kuepuka mambo hayo, bila shaka.

107 Ukichukua, ufungue redio yako, nayo inasema, “Kesho, kutakuwa na baridi, ama, kutakuwa na joto,” chochote redio ingesema. Tutasema, kwa mfano, “Kutakuwa—kutakuwa na joto kesho, kutakuwa na joto,” basi mwangalie maskini huyo nguruwe jike akienda kule na kuchukua vijiti vilivyo upande wa kaskazini mwa kilima, na kuvipeleka upande ule mwingine

wa kilima, usisikilize yale mtangazaji huyo asemayo, hajui anachozungumzia, nguruwe huyo anajua.

¹⁰⁸ Unatoka nje na kuwaangalia sungura hawa wakiingia moja kwa moja chini ya kichaka, na hebu mtu huyo aseme, “Hali ya hewa itakuwa nzuri,” usisikilize anayosema, huyo sungura anajua zaidi ya anavyoweza kujua kuhusu hilo. Mungu amempa njia ya kuepuka mambo hayo, naye anaiamini, na anajiandaa kwa ajili yake.

¹⁰⁹ Kama vile Nuhu alivyofanya na safina, aliitayarisha safina kabla ya mvua yoyote kunyesha. Amina. Mko tayari, alasiri ya leo, kuruka mwondoke? Je, mnaweza kumwona Mungu? Yaondokeeni maradhi haya, na magonjwa, na mashaka, na fadhaa. Mungu yuko katika ulimwengu Wake.

¹¹⁰ Si muda mrefu uliopita, miaka michache iliyopita, mimi na baba tulikuwa tukilima, na ilikuwa ni asubuhi yenye joto, tulikuwa tumelala karibu na mahindi, ndipo—ndipo Baba akasema, “Vema . . .” Farasi wakaanza kukoroma na kukoroma.

Ndipo nikasema, “Wana shida gani, Baba? Kuna mbwa mwitu, ama kitu fulani huko nyuma?”

Akasema, “La, la, dhoruba inakuja.”

Nikasema, “Ati *nini*?”

Kasema, “Dhoruba.”

Nikasema, “Sioni dhoruba yoyote, mahali popote.”

¹¹¹ Akasema, “Billy, hebu kidogo,” kasema, “huelewi.” Akasema, “Mungu amempa farasi silika kwamba wakati dhoruba inakuja,” ninyi nyote mliowahi kumpanda farasi mnaajua jinsi radi itakavyocheza moja kwa moja juu ya manyoya yake, akasema, “ana—ana silika ya kufika mahali pa salama. Hiyo ndiyo sababu anakoroma, wanataka kufika kwenye banda.”

Nami nikasema, “Ati *dhoruba*? Mbona,” nikasema, “hakuna ngurumo, hakuna radi, hakuna wingu, mahali popote.”

Akasema, “Lakini ngoja tu dakika chache.”

¹¹² Sikuwa nimelima raundi mbili, na hii hapa dhoruba ikaja. Mnaona? Mungu aliwapa silika. Mungu yuko katika kila kiumbe, kila mahali, kama tu utaliangalia. Mungu yuko katika ulimwengu Wake. Mnaamini hilo? Bila shaka, Yuko.

¹¹³ Sasa, hapa miaka kadhaa iliyopita, nilikuwa nikisoma makala ambapo kafiri mmoja alivuka nchi nzima. Mwerevu sana, mwenye akili sana, hata wahudumu wasingemkabili. Imekuwa yapata miaka hamsini iliyopita, naye a—alikuwa akiwaongoa watu kutoka Ukristo akawaingiza katika ukafiri. Ndipo hatimaye, afya yake ikadhooifika, naye akaenda Colorado kupumzika. Siku moja alikuwa kambini, naye akatoka, basi akaanza kuangalia miamba hiyo, naye akasema, “Je, ni

kweli, nimekosea? Alifanya—alifanya...? Kuna Mwenye uhai aliyekuweka humo?”

¹¹⁴ Wakati hiyo miti inapopeperushwa huku na huku, na upepo, “Adamu, uko wapi?” Unaona?

¹¹⁵ Basi hatimaye, huyo kafiri akiketi huko nje kwenye gogo akiangalia miamba hiyo alianguka kifudifudi, na kusema, “Nimekosea! Mungu unirehemu, mwenye dhambi!”

¹¹⁶ Si ajabu Maandiko yalisema, “Wakinyamaza, miamba itapiga kelele mara moja.” Jambo fulani litatukia! Kama mtu akiangalia kote katika ulimwengu, anaweza kumpata Mungu. Hivi huamini Mungu yuko katika ulimwengu Wake? Bila shaka, Mungu yuko katika ulimwengu Wake.

¹¹⁷ Sasa tutachukua “Mungu Katika Neno Lake,” kwa dakika moja tu. Ni wangapi wanaoamini Mungu yuko katika ulimwengu Wake? Hakika, Yeye yuko katika ulimwengu Wake. Tungeweza kuendelea alasiri yote, bali hatutaki, tunataka kugusia mambo haya mengine mawili.

¹¹⁸ Sasa, unaweza kumwona Mungu katika ulimwengu Wake? Ni wangapi wanaoweza kumwona Mungu katika ulimwengu Wake? Katika mambo haya yote mbalimbali? Hakika, unaweza. Sasa hebu tuone kama Mungu yuko katika Neno Lake.

¹¹⁹ Mungu yuko katika Neno Lake sana hivi kwamba “Hapo mwanzo kulikuwako Neno, huyo Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili akakaa kwetu.”

¹²⁰ Mungu yuko katika Neno Lake, tunaamini hilo, Yeye hulitimiza. Tunaweza kujua, wakati Mungu anaponena jambo lolote, tunaona Neno hilo likishuka moja kwa moja, imedhihirishwa hasa kile Yeye anachosema kinatimia, kwa hiyo tunajua Mungu yuko katika Neno Lake.

¹²¹ Alimwambia Ibrahimu atampata mtoto kwa Sara, naye akangojea miaka ishirini na mitano, Mungu akatimiza Neno Lake. Akamwambia Nuhu itanyesha, na mambo yote aliyosema, aliwaambia watu mia moja na ishirini ya kwamba, enendeni, mngojee Yerusalemu hata Siku ya Pentekoste itakapotimia, alikuwa anaenda kutuma ahadi ya Baba, alitimiza Neno Lake. Yeye daima hutimiza Neno Lake.

¹²² Alisema, “Mambo haya nifanyayo, ninyi nanyi mtayafanya.” Yeye hutimiza Neno Lake. “Bado kitambo kidogo na ulimwengu,” utaratibu wa ulimwengu, “hautaniona tena, bali ninyi mtaniona, nitakuwa pamoja nanyi, ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari.” Yeye hutimiza Neno Lake. Mungu yuko katika Neno Lake.

¹²³ Hapa, kama nilivyosema hivi majuzi usiku, “Mungu ni... ‘Neno la Mungu ni Mbegu’, Yesu alisema, ‘ambayo mpanzi alienda kupanda, nayo Mbegu hii, ikaota,’ na—na kadhalika.”

Sasa, kila mbegu, kama ni mbegu sahihi, itazaa jinsi ilivyo, itajizaa tena.

¹²⁴ Miaka michache, kama mitatu iliyopita, ama minne, nilikuwa nimeketi kwenye—kwenye duka la vitamutamu nikila a—askrimu pamoja na maskini rafiki yangu mhubiri Mmethodisti, ameenda utukufuni sasa, nasi tulikuwa tumeketi pale tukizungumza juu ya wema wa Mungu.

¹²⁵ Alikuwa ndiye mhudumu mzee yule yule aliyetunga ule wimbo:

Tulilegeza kamba, tulilegeza kamba,
Tukapatana na dhambi.
Tulilegeza kamba, kondoo wakatoka nje,
Lakini mbuzi waliingiaje?

¹²⁶ Ni—nikasema, “Vema, hilo ni rahisi, mlilegeza kamba, hivyo—hivyo tu, mlianza tu kupatana, na hivyo ndivyo mbuzi walivyoingia, wakala Chakula chote cha kondoo.” Nao hawapendi hicho, hawana budi kula na magugu, magugu ya kikanisa. Mbuzi hupata—hupata, hushiba kwa magugu, bali kondoo hana budi kupata Chakula halisi.

¹²⁷ Kwa hiyo angalieni, wakati alipokuwa kule, redio ilikuwa ikitangaza kwenye maskini hilo duka la vitamutamu, Henryville, Indiana, tulimokuwa, alikuwa ni maskini Daktari Spurgeon, rafiki yangu mwema sana, na kwa hiyo redio ilikuwa imefunguliwa, nayo *Majira ya Kilimo* yalikuwa yanaendelea. Na maskini Klabu ya 4-H huko Louisville, Kentucky walikuwa na mtambo kule ambako walikuwa wametengeneza mtambo ambao ungeweza kutoa punje ya mahindi kamilifu sana hata usingeweza kuyatofautisha na yale yaliyokuzwa shambani.

¹²⁸ Kasema ukichukua konzi moja kutoka kwenye gunia la yaliyolimwa shambani, konzi kutoka kwenye gunia la—la yaliyofanywa kwa mashine, uyachanganye pamoja, nawe hungeyatoftutisha tena. Kasema ungeweza kuyapasua, kiasi kile kile cha kalisi, kiasi kile kile cha unyevu, moyo ni sawa kabisa, yangetengeneza unga ule ule wa mahindi, ugali ule ule wa mahindi, bisi zile zile, vivyo hivyo hasa. Kasema kuna njia moja tu ungaliveza kuyatofautisha, hiyo ni kuyazika, ndipo yale yaliyotengenezwa kwa mtambo yataoza yasiishi tena, bali yale yaliyoubwa na Mungu yataishi tena, kwa sababu yana uhai ndani yake.

¹²⁹ Unaweza kumchukua mtu anayeonekana kama Mkristo, anayetenda kama Mkristo, lakini kama mtu huyo hana Neno la Mungu ndani yake, kama hamna chembechembe ya Uhai mle ndani ya kuirutubisha hiyo, kamwe hatafufuka katika ule ufufuo. Hiyo ni kweli. Kwa sababu hawezi kufufuka, hakuna kitu mle ndani cha kumfufua tena, Mbegu.

¹³⁰ Sasa, unapozika mbegu, ninyi wakulima, mnachukua na kutoka hapa nje na kupanda mahindi yenu, hutoki kila

asubuhi na kuifukua, na kusema, “Hebu tuone sasa, je, inakua? Kuna chochote kilichoifanyikia? La.” Unazika tena. Kesho yake baadaye, unasema, “Ninataka kuona kama inaendelea vema,” unaifukua tena; kamwe haitakua namna hiyo. Vema, jambo unalofanya na mbegu, unaitia ardhini, unaifunika, hivyo tu ndivyo unavyoweza kuifanyia, ni juu ya Mungu kufanya yaliyosalia.

¹³¹ Vema, hivyo ndivyo ilivyo na Neno la Mungu. Kama utachukua ahadi yoyote ya Kiungu aliyotoa Mungu katika Biblia Yake, uiweke moyoni mwako, na kuimwagia maji kila siku kwa sifa za Mungu kwamba itatimia, itakua, kama huninii. . .acha kujipumbaza nayo, kama utaiacha tu.

¹³² Usiseme, “Hebu nione, ninaweza kusogeza kidole changu vizuri zaidi leo? Je, ninajisikia vizuri zaidi? Je, maumivu yangu ya kichwa ni afadhali kidogo, ama yote. . .?”

¹³³ Kamwe haitakuwa hivyo, ikabidhi tu kwa Mungu, kisha uondoke, uachane nayo. Hiyo ni Mbegu ya Mungu, itakua.

¹³⁴ Siku moja nilikuwa huko Minneapolis, Minnesota, nami nikapata barua mbaya sana asubuhi hiyo. Na kulikuwa na dhoruba ya theluji usiku huo, nami nikarudi kwenye maskini hoteli ndogo, ya bei rahisi.

¹³⁵ Nami daima hujaribu kukaa mahali. . .Siamini Wakristo wanapaswa kuomba yaliyo mema sana nchini, Mkristo anapaswa kuwa mnyenyekevu. Na—nafikiri ya kwamba, hata kama mngeweza kuyalipia, bado nafikiri tunapaswa kuwa mfano. Bwana wangu hata hakuwa na mahali pa kulaza kichwa Chake, mbweha walikuwa na matundu, na ndege walikuwa na viota, bali Yeye hakuwa na mahali pa kulaza kichwa Chake. Alikuwa ulimwenguni, akaazima hori apate kuzaliwa ndani, akaja kupitia kwenye tumbo la uzazi la kuazima, akaondoka kwenye kaburi la kuazima, jamani, na Mungu wa Mbinguni. Nasi tunapaswa kuonyesha unyenyekevu, pia.

¹³⁶ Kwa hiyo, niliingia na kulikuwa na barua ya kurasa ishirini na mbili kutoka kwa mshauri mmoja wa chuo. Loo, kama hakunishambulia vikali sana! Akasema, “Bw. Branham,” asingeniita *ndugu*, akasema, “Bw. Branham, wazo lenyewe la wewe kusimama mbele ya watu wengi kadiri unavyofanya, halafu theolojia iliyooza hivyo! Sijawahi kusikia hiyo maishani mwangu.” Kisha kasema, “Ulikuwa ukijivunia kuhubiri kwa miaka thelathini na mmoja,” kasema, “kijana, nilikuwa nikihubiri kabla hujazaliwa.”

¹³⁷ Nami nikawazia, “Vema, hiyo ni. . .Hakika ninamheshimu mtu ambaye amekuwa akihubiri kwa muda mrefu hivyo.” Kwa hiyo basi nikasema, “Vema, hilo ni sawa.”

¹³⁸ Kwa hiyo akasema, “Wazo lenyewe ulilosema jana usiku kwamba—kwamba mtumishi wa Mungu. . .” Kasema, “Niliendesha maili kumi na tano kupitia dhoruba ya theluji

inayopofusha kumsikia mtumishi wa Kristo, nami nilipata nini? Ila mpiga ramli aliyeadibishwa.” Vema . . .

¹³⁹ Akasema, “Nawe ulisema ibilisi asingeweza kuponya.” Kasema, “Mtu ambaye angewafundisha watu wengi kadiri unavyowafundisha, wala hajui zaidi ya hayo kuhusu Biblia, wala hajui zaidi ya—ya ibilisi hawezi kuponya!” Kasema, “Nataka uelewe, ya kwamba ninaishi katika jamii hapa, ambapo kuna mwanamke aliye na roho ya uaguzi.” Kasema, “Wanamjia mwanamke huyu, amevaa aproni kubwa, anawapapasapapasa kila mahali namna *hii*, nao wanatia pesa kidogo katika aproni hii.”

¹⁴⁰ Kasema, “Ndipo anang’oa nywele chache kutoka kichwani mwake, na kuchoma mishipa yao, na kuzipaka damu hizi nywele, anashuka kwenye kijito kidogo nyuma yake, na kuzitupa ndani. Watu wanasimama mbele yake, anaenda namna *hii*, na kama analazimika kuangalia nyuma,” mbona kasema, “basi huogonjwa unawarudia watu, usiporudi anautupa kupitia kwake, kwa damu ya watu, na nywele zake mwenyewe, katika kijito.”

¹⁴¹ Kisha kasema, “Tuliandika kumbukumbu yake,” kasema, “angalau asilimia ishirini au thelathini ya hao watu wameponywa. Halafu unataka kuniambia, ya kwamba huamini ibilisi anaweza kuponya.”

¹⁴² Vema, ni—niliwaza tu, “Mshauri wa chuo!” Vema, nikawaza, “Hiyo ni barua nzuri sana, kwa hiyo jambo la kwanza,” nikasema, “Sina budi kumjibu.” Na kama uliwahi kusoma moja ya barua zangu, mimi—mimi ndimi pekee, karibu hivyo, ninayeweza kuisoma.

¹⁴³ Kwa hiyo basi, ni—niliketi chini na kufanya vizuri sana nilivyoweza, nami nikasema, “Ndugu yangu wa thamani,” maana aliniita tu *Branham*, nami ni—nikasema, “Ndugu yangu wa thamani. . .” Nami nilimaanisha hilo, mtu aliyekuwa akihubiri kwa miaka hamsini, anastahili kitu fulani, sasa, ingawa kama amekosea, anastahili kitu fulani.

¹⁴⁴ Nikasema, “Ndugu yangu mpendwa,” nikasema, “jambo la kwanza ninalotaka kusema, kwamba ninakusamehe kwa yale uliyosema, na ninaomba ya kwamba Mungu anakusamehe, pia. Kumbuka, Mafarisayo, waliokuwa wamehubiri kwa muda mrefu zaidi kuliko ulivyohubiri, waliona jambo lilo hilo likifanywa, na kusema ilikuwa ni nguvu za ibilisi, Beelzebuli. Naye Yesu akasema, ‘Ya kwamba wakati lilipofanywa na Roho Mtakatifu katika siku hizi za mwisho, kunena neno moja dhidi yake hakutasamehewa kamwe katika ulimwengu huu, wala ulimwengu ujao.’ Sasa, kwa mfano, vipi kama niko sahihi? Basi miaka yako hamsini ya kuhubiri haina maana. Umeihukumia nafsi yako kuzimu, milele. Kamwe hungesamehewa jambo hilo.” Nikasema, “Ninajua, ndugu, kwamba ulilifanya hilo kwa

kutokujua kwako. Sasa,” nikasema, “usiache hilo liumize hisia zako.”

¹⁴⁵ Lakini nikasema, “Basi ulikuwa ukiendelea kunisukuma kuhusu mimi, theolojia yangu, nikisema ya kwamba ibilisi asingeweza kuponya.” Nikasema, “Nitakupa Yesu. . .” [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Huwezi kuyafanya Maandiko kuwa shaghalabaghala, huna budi kuyaweka wazi na ya moja kwa moja. Hiyo ni kweli. Nikasema, “Yesu alisema Shetani hawezi kuponya, nawe ulisema aliponya.”

¹⁴⁶ Sasa, nikasema, “Sasa, kama utanisamehe,” nikasema, “Ni—nitakupa kile, kuhusu mchawi wenu mliye naye katika ujirani wenu.” Nikasema, “Kama. . .Bila shaka watu hao huponywa, kwa sababu,” nikasema, “huko Afrika, nimewaona wakiziendea sanamu na kuponywa; huko La Salle, Lorraine wana sanamu kule ya mwanamke fulani aliyekufa katika kanisa Katoliki, wanaenda kule na kumwalia mwanamke huyo aliyekufa, wanasema ‘Salamu Maria,’ nao wanaponywa. Hakika, kwa sababu hao watu wanafikiri wanamwenda Mungu kwa njia hiyo, naye Mungu huponya juu ya msingi wa imani, na popote imani inapotimizwa Mungu hana budi kutimiza masharti hayo.” Sawa.

¹⁴⁷ Nikasema, “Kuna watu wengi nchini siku hizi, wanaojiita wenyewe waponyaji wa Kiungu.” Wakisema, ‘Nina nguvu mikononi mwangu. Utukufu! Haleluya! Woooo! Unahisi hiyo?’” Nao Wamarekani wanadanganyika, kama sijui nini, kilegevu sana. Nao—nao—wanafikiri ya kwamba hiyo ni kweli, wanaponywa kwa sababu wao ni. . .Hilo silo. Imani yako iko katika kazi iliyomalizika ya Yesu Kristo, hapo ndipo uponyaji ulipo.

¹⁴⁸ Kamwe usiache mtu yeyote akwambie wana nguvu za kuponya, hawana. Yesu Kristo alikuwa tayari amelipa deni, unawezaje kuikomboa tena? Anakupa risiti dhahiri kutoka kwenye duka la rehani, ulimokuwamo. Umekombolewa kwa Damu ya thamani ya Yesu.

¹⁴⁹ Huna nguvu za kuponya, kitu ulicho nacho ni kuwa na ninii, huenda ukawa na karama ya kumdhihirisha Mungu, huenda ukawa na karama ya kumdhihirisha kupitia kwa mhubiri mashuhuri, kama baadhi ya hawa ndugu zangu, ambao wangeweza kusimama hapa na kufanya kazi hii kuliko vile ningeweza, kwa sababu huo ndio wito wao, wito wangu ni kitu kingine. Lakini kila mmoja wetu ana karama ya kujaribu kukwambia ya kwamba Kristo alikuponya wakati alipokufa kwa ajili yako. *Alijeruhiwa* kwa makosa yako, kwa kupigwa Kwake wewe *uliponywa*. Ni jambo la kukufanya ujue, kama huwezi kuliadini Neno, basi Yeye anatuma ishara na maajabu, na kuthibitisha ya kwamba Yeye ni Kristo aliyefufuka.

Unaona? Kwa hiyo hapo ndipo unapopata uponyaji wako, kwa kumwamini Yeye.

¹⁵⁰ Sasa, kwa hiyo basi, nikasema, “Lakini jambo, ambalo linanitia wasiwasi, Bwana, si hilo, lakini kwamba mshauri wa Chuo cha Kilutheri angeweke fundisho lake juu ya msisimko, ama, juu ya tukio fulani, badala ya kuliweka juu ya Neno la Mungu.” Naam. Loo, unaweza kuwa na namna yoyote ya mhemko, bali hauna budi kuwa ni Neno la Mungu. Hiyo ni kweli. Nikasema, “Mshauri wa chuo, umekuwa ukihubiri kwa miaka hamsini, na ungewekea msingi fundisho lako,” hilo lilimchoma sana, “kuweka fundisho lako juu ya, juu ya namna fulani ya ujuzi ambao mwanamke mmoja alikuwa nao, badala ya kuliwekea msingi juu ya Neno la Mungu! Mungu alisema Shetani hawezi kuponya, na hilo latosha. Anaponena, ni kweli Milele.”

¹⁵¹ Si muda mrefu baadaye, nikapata mwaliko wa kuja nyumbani kwake, Bw. Moore aliambatana nami, maana nilijua mtu huyo alikuwa mwerevu. Na kwa hiyo yeye, baada ya kula chakula cha kutwa huko nje kwenye hicho chuo kikubwa maarufu, nao walikuwa na mamia ya ekari za mahindi, ambapo wanafunzi wangeweza kulima ili kulipia masomo yao, siku hiyo baada ya chakula cha kutwa alisukuma sahani yake nyuma, huyo mshauri wa hicho chuo akaniambia, akasema, “Bw. Branham, tumekuja hapa kukuuliza maswali kadhaa.”

Nikasema, “Huenda nisiweze kuyajibu, bwana.” Nikasema, “Mimi si mwanatheolojia, mimi ni ndugu tu anayewaombea wagonjwa.”

Naye akasema, “Vema . . .” akasema.

¹⁵² Naye Bw. Moore, ambaye ni mwanatheolojia aliketi pamoja nami, basi akasema, “Akikuzidi sana, niguse tu gotini,” kwa hiyo, kwa goti langu.

¹⁵³ Kwa hiyo nilikuwa nimeketi pale, naye akasema, “Bw. Branham, ninaona ya kwamba wewe, nikiyafuatilia maisha yako huko nyuma, wewe ni Mbaptisti.”

Nikasema, “Nilikuwa.”

Naye akasema, “Kukafanyika nini? Kwa nini—kwa nini ukaliacha kanisa la Kibaptisti?”

Nikasema, “Sikuliacha, liliniacha.” Mnaona? Nikasema, “Liliniacha, wakati lilipoukana Ujumbe niliokuwa nikihubiri wa Biblia.”

¹⁵⁴ Naye akasema, “Vema, Bw. Branham, kuna jambo moja ningetaka kukuuliza,” akasema, “ni hili,” akasema, “sasa, kama ulifanya hivyo, ningetaka kusema jambo moja: Ni kitu gani kilichokufanya ujiunge na Wapentekoste?”

Nikasema, “Wanaamini Neno.”

Akasema, “Kwani wana nini?” Kasema, “Nimekuwa huku na kuwaona wakipiga meza mateke na kuangusha viti.”

Nami nikasema, “Loo, hakika. Hiyo ni kweli.”

“Wakibomoa dirisha, ama kitu kama hicho.”

Nikasema, “Hakika.”

Kasema, “Ni kitu gani?”

Nikasema, “Roho Mtakatifu.”

Naye akasema, “Ati Roho Mtakatifu?”

Nikasema, “Hakika, kama hawatalifanya gurudumu lizinguke vizuri, hawana budi kuupuliza utoke kwenye filimbi mahali fulani, wana mvuke mwingi,” nikasema.

¹⁵⁵ Na huo ndio ukweli. Kama kanisa hili la Kipentekoste lingechukua sifa zake nyingi na kuzifanyia kazi, lingefanya kitu kwa ajili ya Ufalme wa Mungu. Mungu amewapa Roho Mtakatifu, mnapenda kupaza sauti kupaza sauti kwa Yeye, na kusifu kwake Yeye, lakini wekeni tu hilo katika karama na maajabu, kisha mtoke kwenda mtaani na kuwaingiza wenye dhambi, na mambo kama hayo, kanisa lenu litakua, na kila kitu kitaenda sawa. Msiupulize utoke kwenye filimbi, uwekeni katika matendo na muuache, mviringishe gurudumu, garimoshi la Injili.

¹⁵⁶ Ndipo akasema, “Vema, unafikiri sisi Walutheri tuna nini? Unafikiri kwamba...? Tunaamini ya kwamba tunampokea Roho Mtakatifu tulipoamini.”

¹⁵⁷ Nikasema, “Paulo angetofautiana nanyi katika Matendo 19, yeye alisema, ‘Je, mmempokea Roho Mtakatifu *tangu* mlipoamini.’ Kamwe hakusema, ‘Sasa, pitisha hilo katika Kiyunani, Kiebrania, ama chochote utakacho.’ Ni, *tangu* mlipoamini.”

¹⁵⁸ Sasa, wanaamini... Kanisa letu la Kibaptisti lilifundisha unampokea Roho Mtakatifu unapoamini, bali si kweli. Paulo alisema, “Ninyi, mmempokea Roho Mtakatifu *tangu* mlipoamini.” Nao hao watu walikuwa wakipaza sauti, mbona, Akila na Prisila, walikuwa na mikutano mikuu, na kila kitu kilikuwa kikiendelea, lakini akasema, “Je, mmempokea Roho Mtakatifu *tangu* mlipoamini?”

Wakasema, “Hatujui kama kuna Roho Mtakatifu.”

¹⁵⁹ Paulo alipokwisha kuwabatiza tena, na kuwawekea mikono, na Roho Mtakatifu akaja juu yao, walinena kwa lugha na kutabiri, ndipo wakampokea Roho Mtakatifu.

¹⁶⁰ Kwa hiyo akasema, “Unafikiri sisi, Walutheri, tuna nini?”

¹⁶¹ Nikasema, “Kwa uwezekano, nafikiri mko sawa.” Akasema... Nikasema, “Hebu niwape tu mfano mdogo, kwa sababu sijui hasa.” Nikasema, “Sasa, mnafanya nini hapa? Mnatoka nje na kulima shamba lenu wakati wa majira ya

kuchipua, mnang'oa mashina yote humo, mnapanda mahindi yenu. Kesho yake asubuhi mnatoka na muda si muda, mnasema... Kuna matawi mawili madogo yanayochipuka kwenye mahindi, majani mawili madogo. Sasa, tuseme unaangalia nje na kuona hayo machipukizi madogo yakija, unasema, 'Bwana asifiwe! Nina zao la mahindi.'" Nikasema, "Je, una zao la mahindi?"

Akasema, "Vema, sijui unachozungumzia."

¹⁶² Nikasema, "Kwa uwezekano, una zao la mahindi," nikasema, "hilo lilikuwa ni ninyi Walutheri, yale marekebisho ya kwanza. Ndipo basi muda si muda mwajua, ubua huo ukakua, majani haya yakawa makubwa, na muda si muda mwajua, ukaingia kwenye kishada, huyo alikuwa ni John Wesley kwenye yale marekebisho ya pili, utakaso, kazi ya pili dhahiri ya neema. Basi ilifanya nini?"

¹⁶³ Nikasema, "Kishada kiliangalia nyuma kwenye ubua, na kwenye jani, na kusema, 'Sina haja nanyi, tumetakaswa, ninyi ni Walutheri tu.'" Ndipo nikasema, "Baada ya kitambo kidogo chavua ikatoka, na kuanguka kwenye jani la ngano, kisha ikatokea, na ilikuwa na suke, punje ya mahindi juu yake," nikasema, "hiyo ilikuwa Wapentekoste."

¹⁶⁴ Nikasema, "Ndipo Mpentekoste akaangalia juu, na kusema, 'Sina haja na yeyote wenu.'" Lakini nikasema, "Hata hivyo, uhai ule ule uliokuwa katika yale majani mawili madogo ulifanya kishada, na pia ukafanya punje." Kweli. Nikasema, "Sisi. . ."

¹⁶⁵ Mnaona, Pentekoste ni kurudishwa, Pentekoste ina Roho Mtakatifu, bali ni kurudishwa kwa karama. Punje ile ile, Yesu yeye yule aliyeingia ardhini anajizaa Mwenyewe, anakuja kupitia kwenye ubua, na sasa anajizaa Mwenyewe katika utimilifu katika punje za asili, kama alivyoshuka chini." Amina.

Akasema, "Ungetuitaje?"

¹⁶⁶ Nikasema, "Kanisa la Kipentekoste ni kanisa la Kilutheri lililoendelea." Hiyo ni kweli. Kweli kabisa. Ni Walutheri walioendelea, nao Wanazarayo, na Pilgrim Holiness, na wote, ni Kanisa tu lililoendelea. Nikasema, "Nitakubali tuna kuvu nyingi sana kwenye suke, lakini tuna punje kidogo mle, pia, Mungu asifiwe. Ni—ni la asili."

¹⁶⁷ Mungu yuko katika Neno Lake, nalo Neno ni Mbegu, haidhuru ni kitu gani kinachotukia litakua, hata hivyo. Mungu alisema litakuwako bila waa wala kunyanzi. Mnaamini Mungu yuko katika Neno Lake? Mungu huchukua Neno Lake, Mungu hutimiza Neno Lake, Mungu hutimiza ahadi Yake ya Neno Lake. Kile afanyacho, anakifanya. Mungu yuko katika ulimwengu Wake. Amina? Mungu yuko katika Neno Lake. Mnaamini hilo?

¹⁶⁸ Sasa "Mungu Katika Mwanawe," niliandika hapa chini, "Mungu Katika Mwanawe." Vema. Je, Mungu yuko ndani ya

Mwanawe? Biblia ilisema Yeye alikuwa, “Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake.”

¹⁶⁹ Sasa, kama ninyi wa Umoja, Uwili, Utatu, Unne, na chochote ulicho, mtaingiza tu jambo hili niani mweni sasa hivi, m—mngepeana mikono, na kusema, “Sisi ni ndugu.” Tazama, Mungu alikuwa ndani ya Kristo akiupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake. Yesu alikuwa Mwana wa Mungu, ambapo Mungu alimtia uvuli Mariamu, akaumba katika tumbo la uzazi Seli ya Damu.

¹⁷⁰ Sasa, mmewasikia watu wakisema, “Tuliokolewa kwa damu ya Kiyahudi.”

Hatungeweza kuokolewa kwa damu ya Kiyahudi, ina dhambi tu kama damu nyingine yoyote.

“Tuliokolewa kwa damu ya Mataifa?”

¹⁷¹ La, bwana, hata hatukuokolewa kwa damu ya binadamu, tuliokolewa kwa Damu ya Mungu, Damu ya Mungu. Che—chembechembe ya uhai hutoka kwenye seli ya damu, nayo Seli ya Damu hapa ilitoka kwa Mungu Muumba, Ambaye aliumba Seli ya Damu iliyomzaa Mwana wa Mungu.

¹⁷² Wakati mwabuduo wa kale alipomchukua mwana-kondoo, akaenda madhabahuni kuabudu, alimweka juu pale, akamwekea mikono, na kukiri dhambi zake, wakakata koo yake, wakavunja seli ya damu, huyo mwana-kondoo akafa. Sasa, aliondoka moja kwa moja akiwa na hali ile ile aliyokuwa nayo alipoingia. Dhambi zake zilisamehewa, aliondoka na tamaa ile ile, kama alikuwa ameiba, amepiga risasi, amefanya uzinzi, chochote kile, alirudi akiwa na tamaa ile ile. Lakini kama mtu akiweka mikono yake juu ya kichwa cha Mwana wa Mungu!

¹⁷³ Kwa nini hakwenda—hakwenda kama vile angeenda kama angeweka mikono yake juu ya Mwana wa Mungu? Chembechembe ya damu kutoka kwa mwana-kondoo huyo ilikuwa na uhai wa mnyama ndani yake, nao uhai wa mnyama hautaendana na uhai wa mwanadamu, kwa hiyo wakati huo uhai uliporudi, ulikuwa ni uhai wa mnyama kwa uhai wa mwanadamu, wala usingeweza kumsaidia chochote. Lakini wakati Chembechembe ya Damu ya Mungu ilipovunjwa, Roho wa Mungu anayeishi katika Seli hiyo, anaporudi katika umbo la Roho Mtakatifu, huyo mwanadamu yuko huru na dhambi, dhamiri yenyewe ya dhambi imehukumiwa. Amina. Ninaamini hilo kwa moyo wangu wote.

¹⁷⁴ “Mwabuduo akiisha kutakaswa mara moja hana tamaa ya dhambi tena.” Biblia inasema *ufahamu*, ambalo kwa kweli linamaanisha “shauku.” Mwabuduo akiisha kuweka mikono yake juu ya kichwa cha Yesu Kristo kwa imani, na kuuhisi huo mwili unaotetemeka, kama vile mtu alivyofanya kwa mwana-kondoo, akifa, akilia, Yeye asiye na hatia, na kwa moyo wako wote, ukiamini kwamba Mwana wa Mungu alikufa mahali

pako, basi unapofanya maungamo hayo Roho Mtakatifu, kutoka kwenye Seli hiyo ya Damu iliyokutakasa, anaingia maishani mwako, nawe ni kiumbe kipya katika Kristo Yesu, Uzima wa Mungu uko ndani yako, Naye amekukubali, nawe ni Mwana wa Mungu. Amina. Msio gope, *amina* maana yake ni “na iwe hivyo,” hilo halitakudhuru.

¹⁷⁵ Angalieni, Mwana wa Mungu, Roho wa Mungu, yuko ndani ya Mwanadamu, kwa hiyo Mungu alikuwa ndani ya Kristo akiupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake. Mungu ni Roho, hakuwa na mikono mpaka alipofanyika Yesu, hakuwa na miguu, mikono, miguu, na kadhalika, mpaka alipofanyika Yesu, alidhihirisha. “Hakuna mtu aliyemwona Baba wakati wowote, bali Mwana wa Peeke amemfunua.” Yeye, Mungu, aliishi katika mwili wa Kristo.

¹⁷⁶ Linapaswa kuwa ni la kushangaza, linapaswa kumfanya mwanadamu kushangaa. Angeweza kushuka kutoka Mbinguni, moja kwa moja kwenye ushoroba wa Mbinguni, pamoja na gwaride zima la Malaika kama angetaka, angeweza kuzaliwa mtu mzima kabisa, angeweza kushuka na fahari na utukufu wote wa Mbinguni, bali hakuchagua hilo, alikuja kwenye zizi, akazaliwa juu ya lu—lundo la samadi. Na maskini Yehova akilia horini, mtoto Yehova akicheza kama mvulana, maskini Yehova akifanya kazi kwa bidii kama mwanadamu. Yeye—Yeye aliunganisha tabaka Lake pamoja nasi, Mungu akawa mwanadamu.

¹⁷⁷ Wakati Yesu Kristo alipozaliwa, Mungu alikuwa mwanadamu duniani, akimdhihirisha Mungu, kile alichokuwa, alifanya kazi na kushughulika, na kuhurumia tineja, a—alipitia kila jaribu tunalopitia. Mungu alifanya hivyo, apate kuipa haki hukumu Yake Mwenyewe. Yeye, hukumu Yake, hapana budi kuwe na haki. Kama hakuna haki, kuna faida gani kufanya hukumu? Na kama hakuna hukumu bila adhabu, basi si hukumu, bado.

¹⁷⁸ Kwa hiyo, alipata adhabu ya hukumu Yake Mwenyewe, na akafa kama mwenye dhambi, kuihukumu dhambi ya ulimwengu, ili sisi, kwa haki Yake, tupate upatanisho wa kurudi kwenye Kiti cha Enzi cha Mungu katika ushirika, kama tulivyofanya katika bustani ya Edeni. Endapo hiyo siyo Injili, siujui. Hiyo ni kweli kabisa. Mwana wa thamani wa Mungu. Hakika, Mungu alikuwa ndani ya Mwanawe.

¹⁷⁹ Si kuita dini zozote mbalimbali, siwakilishi yoyote ya hizo, ninaziwakilisha zote. Hapa wakati fulani uliopita, nilikuwa kwenye Ukumbi wa Robinson huko Little Rock. Kulikuwako na mzee aliyekuwa kwenye mikongojo, alikuwa amepambanuliwa, aliua penseli pembeni kwa miaka mingi, alikuwa Mnazarayo. Kesho yake, alikuwa akishuka mtaani ameshika hii mikongojo

ya kale, akisema, “Maskini rafiki zangu, nimemalizana nayo,” akishuhudia.

Usiku huo, nilikuwa, nililingia mimbarani kuhubiri, naye akasema, “Hebu kidogo, Bw. Branham!”

Nikasema, “Naam, bwana.”

¹⁸⁰ Alikuwa juu kwenye roshani, naye akasema, “Unajua, nilipokusikia ukihubiri, nilikuwa na hakika ulikuwa Mnazarayo,” naye akasema, “kwa sababu unahubiri utakatifu,” halafu akasema, “kisha nasikia mtu fulani akiniambia ulikuwa Mbaptisti, karibu watu hawa wote ni Wapentekoste,” Kasema, “Sielewi hilo.”

Nikasema, “Loo, baba, hilo ni rahisi,” nikasema, “Mimi ni Mpentekoste, Mnazarayo, Mbaptisti.”

Ja—jambo ndilo hilo. Sisi ni wawakilishi wa Yesu Kristo, jambo ndilo hilo, sio dhehebu lako, Mungu wako.

¹⁸¹ Sasa, mwanamke huyu alikuwa mfuasi wa kanisa la Christian Science, mama mzuri sana, naye akasema, bila shaka, hawaamini katika, Yesu kuwa ni Mungu, akasema, “Bw. Branham, ninafurahia mafundisho yako, lakini,” kasema, “kitu pekee kinachoifanya damu yangu kutetemeka ni wewe kujaribu kumfanya Yesu kuwa Mungu.” Kasema, “Unamjivunia kupita kiasi.”

Nikasema, “Siwezi kujivuna vya kutosha juu Yake.”

Akasema, “Vema, daima unamjivunia, unamjivunia.”

Nikasema, “Yeye...Mimi, kama nilikuwa na ndimi elfu kumi, nisingeweza kumjivunia vya kutosha,” nikasema, “kile Yeye alichonifanyia.”

Akasema, “Lakini unamfanya Mungu.”

Nikasema, “Yeye alikuwa ni Mungu. Kama hakuwa Mungu, ulimwengu wote umepotea.” Hiyo ni kweli kabisa.

Akasema, “Kama nikiiniii...Ulisema, ulikuwa wa kimsingi, ulidumu tu na Biblia.”

Nikasema, “Hiyo ni kweli.”

Akasema, “Kama nitakuthibitishia kwa Biblia yeye hakuwa Mungu, utakubali?”

Nikasema, “Kama Biblia ilisema Yeye hakuwa, ningekubali.” Nikasema, “Lakini Biblia haisemi hivyo.”

Akasema, “Loo, naam, pia!”

Nikasema, “Iko wapi?”

¹⁸² Akasema, “Vema, na ni wa Kwanza...katika Yohana Mtakatifu mlango wa 11, wakati Yesu alipokuwa akishuka kwenda kwenye kaburi la Lazaro, Biblia ilisema alilia.” Kasema, “Bw. Branham, asingeweza kulia na awe ni Mungu.”

¹⁸³ “Mbona,” nikasema, “mama, hoja yako ni nyembamba kuliko mchuzi uliotengenezwa kwa kivuli cha kuku aliyekufa kwa njaa.” Nikasema, “Vema, wewe...Vema, hayo si Maandiko.” Nikasema, “Angalia hapa, Yeye alikuwa Mungu *na* mwanadamu pia.” Nikasema, “Yeye alikuwa mwanadamu, wakati alipolia, kwenye kaburi la Lazaro, lakini wakati alipoyainua maskini mabega Yake juu, na kusema, ‘Lazaro, njoo huku,’ na mtu aliyekuwa amekufa siku nne, akasimama kwa miguu yake na kuishi tena, hilo lilihitaji zaidi ya mwanadamu, hilo lilihitaji Uungu kufanya hivyo. Mungu alikuwa ndani ya Kristo.”

¹⁸⁴ Alikuwa ni mwanadamu akishuka kutoka kilimani usiku ule, akiwa na njaa, akiangalia chini, ama asubuhi ile, hasa, akitafuta chakula kwenye huo mtini asipate chochote, alikuwa mwanadamu wakati alipokuwa na njaa, lakini wakati alipochukua biskuti tano na samaki wawili na kuwalisha watu elfu tano, huyo alikuwa ni zaidi ya mwanadamu, huyo alikuwa ni Mungu akiishi ndani ya mwanadamu. Hakika ilikuwa hivyo.

¹⁸⁵ Alikuwa mwanadamu wakati alipokuwa amechoka, amelala kwenye maskini ule mtumbwi mdogo huko nje usiku ule, nguvu zilikuwa zimentoka kutokana na maono na kadhalika siku nzima. Naye ibilisi akaapa usiku huo, labda elfu kumi miongoni mwao wa baharini kwamba wangemzamisha, naye Huyo hapo kwenye ile meli ndogo huko nje, akirushwa huku na huku kama kizibo cha chupa katika dhoruba kwenye bahari kuu. Huyo hapo akielea namna hiyo, huku Yeye amelala nyuma ya chombo, mawimbi hata hayakumwamsha, amelala, kwa hiyo alikuwa amechoka na amedhoofika.

¹⁸⁶ Alikuwa mwanadamu wakati alipokuwa amelala, lakini mara alipoamshwa, haleluya, loo, aliweka mguu Wake kwenye demani ya hicho chombo, na kusema, ‘Amani tulia,’ nao upepo ukaingia kwenye ghuba zake ndogo kama mtoto mchanga kwenye ninii yake. . . Upepo na mawimbi yalimtii, hilo lilihitaji zaidi ya mwanadamu kufanya hivyo, hilo lilihitaji Mungu. Hilo lilihitaji uvuvio, hilo lilihitaji nguvu za Uungu kufanya hivyo. Mungu alikuwa ndani ya Mwanawe. Mnaamini hilo?

¹⁸⁷ Alipokwisha kufa msalabani, kweli alilia apate rehema, Yeye alikuwa mwanadamu, alikuwa akililia rehema msalabani, lakini kwenye asubuhi ya Pasaka, wakati alipofufuka na kuvunja mihuri ya mauti na kuzimu, na kufufuka tena kutoka kaburini, Yeye alikuwa ni zaidi ya mwanadamu. Inahitaji zaidi ya mwanadamu kufufuka kutoka kaburini, inahitaji Mungu kufanya hivyo.

Si ajabu mshairi alisema:

Alipoishi, Yeye alinipenda; akifa, Yeye aliniokoa;

Alipozikwa, alizipeleka dhambi zangu mbali sana;

Alipofufuka, alinihesabia haki bure milele:

Siku moja Yeye yuaja—loo siku tukufu!

¹⁸⁸ Naam, bwana. “Ndani Yake mlikaa utimilifu wote wa Mungu kwa jinsi ya mwili. Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake.”

¹⁸⁹ Mnaamini Mungu yuko katika ulimwengu Wake? Mnaamini Mungu yuko katika Neno Lake? Mnaamini Mungu alikuwa ndani ya Mwanawe? Sasa jambo linalofuata nililo nalo hapa ni “Mungu Katika Watu Wake.”

¹⁹⁰ Sasa tutaona kama tunaweza kumleta kwa watu Wake. Mungu ni Roho, Naye daima amemtumia mwanadamu kujidhihirisha Mwenyewe duniani, alifanya hivyo katika Mwanawe.

¹⁹¹ Alikuwa, Mungu alikuwa ndani ya Daudi. Mlijua hilo? Mungu alikuwa ndani ya watu Wake. Daudi, alipokuwa mfalme aliyekataliwa, alipanda juu ya kilima, akaangalia nyuma, akilia kama mfalme aliyekataliwa. Miaka mia tano baadaye, mwana wa Daudi aliketi kwenye kilima kile kile kama Mfalme aliyekataliwa, na akaulilia Yerusalemu. Hiyo ni kweli?

¹⁹² Yusufu alikuwa na Kristo ndani yake, wakati alipozaliwa ndugu wa kiroho. Ndugu zake wengine walimchukia, angalia kanisa hilo leo, hao ndugu wengine walimchukia bila sababu. Alipendwa na baba yake, akachukiwa na ndugu zake. Sasa, walimchukia bila sababu, asingeweza kujizuia kwa sababu alizaliwa kuona maono na kufasiri ndoto, bali walimchukia, wanafanya hivyo leo, jambo lile lile.

¹⁹³ Ibilisi humchukua mtu wake, bali kamwe si roho yake; Mungu humchukua mtu Wake, bali kamwe si Roho Wake. Roho aliyekuwa juu ya Eliya alikuja juu ya Elisha, na kutoka kwa Elisha hadi kwa Yohana Mbatizaji, na kutabiriwa kuja tena katika siku za mwisho. Mnaona? Mungu alimtoa Roho kutoka kwa Mwanawe, akamrudisha kwa Kanisa.

¹⁹⁴ Mungu humchukua mtu Wake bali kamwe si Roho Wake; ibilisi humchukua mtu wake, bali kamwe si roho yake. Hizo roho mbili zimepigana katika mwili wa mwanadamu tangu mwanzo wa wakati, hiyo ni kweli, nao watafanya vita hata mwisho. Kama tu ukisoma Maandiko na kuangalia jinsi zinavyofanya kazi, hutapotea, kama utamkubali kama Mwokozi wako, na kama Kiongozi wako akuongoze katika Maandiko chini ya... tunaposafiri juu ya barabara kuu ya maisha katika gome lako dogo. Mwache aingie pamoja nawe na kuiendesha meli yako.

¹⁹⁵ Sasa, tunaona Mungu alikuwa ndani ya Musa, Mungu alikuwa ndani ya Eliya. Huyu hapo Eliya, mtu aliyekuwa amelala huko nje kwenye—kwenye pango huko nje. Yule mwanamke Mshunami ambaye alikuwa amembariki, naye akapata mtoto,

kisha huyo mtoto akafa, ndipo Eliya akajitokeza jukwaani. Eliya alikuwa mtu wa Mungu. Alipoingia mtoto mchanga alikuwa amelazwa kitandani mwake.

¹⁹⁶ Kwanza, Eliya alijua ya kwamba alikuwa ni mtu wa Mungu, hakujigamba kuhusu jambo hilo, na kujisifu kulihusu, bali alijua alikuwa ni mtu wa Mungu. Kwa hiyo, alikuwa ametembelea fimbo hii kuukuu, naye akasema, akamwambia Gehazi, “Chukua fimbo hiyo uende ukaiweke juu ya mtoto huyo mchanga.” Alijua ya kwamba kila kitu alichogusa kilibarikiwa, kwa sababu Mungu alikuwa ndani yake. Laiti angaliweza kumfanya mwanamke huyo kuamini jambo lile lile!

¹⁹⁷ Hivyo ndivyo yule mwanamke alivyogusa upindo wa vazi la Yesu, kwa sababu alijua Yeye alikuwa ni Mtu mtauwa, kwamba Mungu aliishi ndani ya watu Wake. Naye alijua kama Mungu alikuwa ndani ya Eliya, hakika Yeye alikuwa ndani ya Yesu. Alijua ya kwamba . . .

¹⁹⁸ Kama sisi Wapentekoste tungeweza kuheshimiana namna hiyo, tukijua ya kwamba kamwe tusingesengenyana, tungekuwa ndugu, tungekuwa dada, kusingekuwa na fedheha kamwe miongoni mwetu, kama tungeweza kutambuana kile tulicho: wana na binti za Mungu. Naye Mungu anaishi katika Kanisa Lake, ndani ya watu Wake. Bila shaka, ndivyo ilivyo. Mungu yuko ndani ya watu Wake. Mnaamini hilo?

¹⁹⁹ Mwangalieni nabii huyu, mwanamke huyo hakuamini ile fimbo. Nafikiri hapo ndipo Paulo alipopata lesa kuchukuliwa kutoka mwilini mwake, maana ninaamini Paulo asingehubiri chochote ila kile kilichokuwa katika Neno, kwa hiyo akawatumia watu hizo lesa. Mungu alikuwa ndani ya Paulo, nao watu walikuwa wamechukua lesa kutoka katika mwili wa Paulo, wakaziweka juu ya miili yao, nao pepo wakawatoka, na magonjwa yakaponywa. Mungu alikuwa ndani ya mwanadamu. Mnaamini hilo? Paulo.

²⁰⁰ Mungu alikuwa ndani ya Eliya, akamwita jukwaani pa mtoto mchanga aliyekufa. Hakujua la kufanya, huyo mtoto alikuwa amekufa, kwa hiyo akatembea tu huku na huku, huku na huku sakafuni. Loo, napenda hilo! Akimngojea Roho Mtakatifu aje, akitembea huku na huku chumbani. Ndipo baada ya kitambo kidogo, akaanza kuhisi Roho akija juu yake. Ninaamini alifanya hima kidogo, mwajua, akitembea upesi kidogo. Loo, alimhisi Roho, akajilaza juu ya huyo mtoto mchanga, naye huyo mtoto akapiga chafya mara saba akafufuka. “Mungu Katika Watu Wake.”

²⁰¹ Ni kitu gani kingeweza kurejesha uhai kutoka mautini, ila Mungu! Amina. Whiu! Ninajisikia kubarikiwa sana sasa hivi. Loo, jamani, kwani mnafikiri Mbaptisti hapigi makelele? Hakika ninayapiga. Loo, “Mungu Katika Watu Wake.”

²⁰² Kulikuwako na mzee mvuvi, hakuwa na...Siku hizi tunawaangalia wenye akili, yule jamaa mkubwa ambaye amepitia chuoni na anajua digrii zote, na kupata D.D.D., na ma-Ph.D., na kila namna ya ma-D.D. Na kwa hiyo basi, muda si muda mwajua, anafika kule juu, mwajua, naye anajua yote kulihusu, tunawazia, “Huyo ndiye yule jamaa!” Lakini Mungu alimweka maskini mvuvi mzee, wakati mmoja, chini ya mamlaka Yake, asingeweza hata kuandika jina lake mwenyewe, asiye na elimu, asiye na maarifa, nao watu wakamwona Mungu akitenda kazi katika mtu huyo, mpaka kweli wakakaa kwenye kivuli cha huyo mvuvi na wakaponywa, kila mmoja aliyepitiwa na kivuli Chake.

²⁰³ Mungu yuko ndani ya watu Wake. Mnaamini hilo? Mungu yuko katika ulimwengu Wake. Mnaamini hilo? Mungu yuko katika Neno Lake. Mnaamini hilo? Mungu yuko ndani ya Mwanawe. Mnaamini hilo? Mungu yuko ndani ya watu Wake. Mnaamini hilo?

²⁰⁴ Angalieni, jana usiku, tulipokuwa tukizungumza juu ya, “Kazi nizifanyazo Mimi, ninyi nanyi mtazifanya,” tulichukua kazi alizofanya, na kuonyesha zilikuwa ni gani, aliahidi angekuwa hapa.

Mnasema, “Lakini Mungu aliishi katika wakati mwingine.”

²⁰⁵ Mungu anaishi milele, Mungu ni wa Milele, Mungu hawezi kufa. Mungu... Waliuua ule Mwili, Yesu, bali Mungu akaufufua tena, Naye yu hai milele, Roho Wake anaishi ndani ya Kanisa leo. Roho Wake yuko hapa sasa, Roho Wake yuko miongoni mwa watu Wake. Yeye hujithibitisha Mwenyewe, si kwa ninii fulani... Angeweza kujithibitisha kuwa *hai* kwa hili, angeweza kujithibitisha Mwenyewe kuwa hai kwa kutua kwa jua, angeweza kujithibitisha Mwenyewe kuwa hai kwa Neno Lake, Angeweza kujithibitisha Mwenyewe kuwa hai kwa Roho Wake aliye humu jengoni sasa, na wanaume na wanawake ambao watajikabidhi Kwake. Amina.

Hebu ujikabidhi Kwake, useme, “Ni nini hutendeka, Ndugu Branham, unapoona hayo maono?”

²⁰⁶ Si kitu ulimwenguni, ila kuwa tu na karama ya kujua jinsi ya kujituliza, kumweka *William Branham* kando. Huyo ndiye adui mkubwa sana niliye naye ni *William Branham*, sikuzote ananipinga, daima anamzuia Mungu, nitasema. Yeye, daima humzuia Mungu, Yeye amechoka kupita kiasi, hataki kufanya *hivi*, hataki kufanya *vile*. Kama ninaweza tu kumsulubisha jamaa huyo, Mungu anaweza kuutumia, Mungu anaweza kuutumia mwili huu.

²⁰⁷ Hii hapa maikrofoni, hii ni bubu mpaka niizungumzie, ama mtu fulani anene ndani yake, bali haiwezi kujinenea. Mtu angewezaje kuona ono? Mtu angewezaje kumponya mgonjwa? Kuwekea mikono kunawezaje kumfufua mtoto aliyekufa, au

kadhalika? Kutafanyaje hivyo kamwe? Si mwanadamu, ni Mungu ndani ya mtu huyo, sawa tu na Mungu katika kutua kwa jua. Mungu yuko kila mahali.

²⁰⁸ Tunataka kuzaliwa kwa Roho Wake, na kumtambua, kumtazamia. Yuko karibu sana nanyi, Yeye hayuko tu karibu nanyi, ninyi watu mliozaliwa mara ya pili, tayari yuko ndani yenu, akijaribu kufanya ninii Yake. . .

²⁰⁹ Naye ibilisi amesimama pale akisema, “Usiamini, usiamini, usiamini, *hivi, vile*. Si kwa ajili yako, sivyo, kwa ajili ya siku nyingine.”

Loo, sema, “Rudi nyuma yangu, Shetani. Imeandikwa, ‘Kazi nizifanyazo Mimi, ninyi nanyi mtazifanya.’”

²¹⁰ Hivyo ndivyo Yesu alivyomshinda Shetani, Yeye kamwe hakutumia nguvu Zake, Yeye alikuwa ni Mungu aliyedhihirishwa katika mwili, bali hakutumia nguvu Zake. Karama zote zilizokuwako Mbinguni, Yeye alikuwa nazo ndani Yake, bali hakuzitumia hizo, Yeye alichukua tu Neno la Baba, Akasema, “Imeandikwa, utamsujudu Bwana Mungu wako. Imeandikwa! Imeandikwa! Imeandikwa! Imeandikwa!” Naye akamshinda Shetani. Nalo Neno la Mungu litamshinda Shetani mahali popote kwa misingi yoyote chini ya hali zozote, Neno Takatifu la Mungu.

²¹¹ Mungu anaishi katika ulimwengu Wake, Mungu aliishi katika Neno Lake, Mungu anaishi katika Mwanawe, Mungu anaishi ndani ya watu Wake, Yeye ni Mungu kila mahali. Mkimruhusu tu aingie sasa, mtamwona Mungu akiishi tena alasiri ya leo miongoni mwetu.

Na tuinamishe vichwa vyetu.

²¹² “Kwa kuwa Neno la Mungu lina ukali, lina nguvu zaidi, kuliko upanga uwao wote ukatao kuwili, tena huchoma hata kugawanya, na mafuta ya mfupa, Huyatambua mawazo na makusudi ya moyo,” Neno la Mungu huingia ndani ya mwanadamu na kutambua wazo. Yesu alitambua mawazo yao. Kama hiyo ni kweli, semeni, “Amina.” Yeye alikuwa nini? “Hapo mwanzo alikuwako Neno, huyo Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno akafanyika mwili.” Naye akasema, “Mnanihukumu Mimi kwa sababu ninajiita Mwenyewe Mwana wa Mungu, huku imeandikwa katika torati zenu ya kwamba ninyi ni miungu.”

²¹³ Mwanadamu alifanywa kuwa mungu, milki yake ni dunia. Dunia nzima inangojea sasa kule kudhihirishwa kwa wana wa Mungu kudhihirishwe. Angalieni jinsi tulivyo nyuma sana. Lakini kumbukeni, manabii, Yeye alisema, “Kama mnawaita miungu, waliojiliwa na Neno la Mungu. . .”

²¹⁴ Nabii alikuwa nani? Mfasiri wa Kiungu wa Neno, alikuwa na tafsiri ya Kiungu. Ishara za Yeye kutabiri na kujua tangu

zamani, hizo zilikuwa ni kuwathibitishia watu ya kwamba alikuwa ni Nabii.

²¹⁵ Hivyo ndivyo Myahudi anavyosema, “Hebu tumwone akiichukua Biblia hii, inasema, ‘Ya kwamba Yesu alikuwa ndiye Kristo na alikufa na kufufuka tena, mambo niliyofanya ninyi nanyi mtayafanya.’ Hebu tumwone akifanya ishara ya nabii, tutaamini ya kwamba huyo ni Roho.”

²¹⁶ Huyu alikuwa ni Masihi, Naye anatenda kazi katika mtu Wake tena, ni nabii Wake. Mnaona? Anafanya kazi katika hilo. Inawezaje kufanywa? Na Mungu pekee. Mungu Ndiye pekee anayeweza kufanya hivyo.

²¹⁷ Je, unataka kukumbukwa katika maombi? Inua mkono wako, useme, “Mungu, unirehemu, sasa nataka kumwamini Bwana Yesu kwa moyo wangu wote. Ninajua ya kwamba mimi ni kiimbe ambacho—ambacho kimefungamana na Umilele.”

²¹⁸ Kulikuwa na wakati mmoja ambapo hukukuwako na kitu, mahali popote, lakini hakutakuwako na wakati ila ule ambapo wewe utakuwa kitu fulani ama mahali fulani. Kama wewe ni mwenye dhambi, fanya uamuzi wako alasiri ya leo. Kristo yuko hapa kukusaidia, kukuokoa. Je, waweza...? Sipendi sana kuwashawishi watu madhabahuni. Nafikiri kama Neno la Mungu halitafanya hivyo... Yesu alisema tamshi hili, usiache likudhuru, “Wote alionipa Baba, watakuja Kwangu. Lakini hakuna mtu awezaye kuja, asipovutwa na Baba Yangu kwanza.” Tunatupa tu jarife.

²¹⁹ Je, wewe ni mwenye dhambi? Ungetaka tu kuinua mikono yako? Sikuiti madhabahuni, sema tu, “Ndugu Branham, mimi ni mwenye dhambi, nitamwinulia Mungu mikono yangu. Mungu nifanye halisi, hata niweze kukuona Wewe kama yule mvuvi wa kale, ninataka kukuona Wewe kote katika ulimwengu Wako, katika Neno Lako, nataka kukuona Wewe.” Inua mkono wako, useme, “Niombee, ndugu.” Mungu akubariki. Mtu mwingine, inua mkono wako. Mungu akubariki. Mungu akubariki huko nyuma. Mungu awabariki.

²²⁰ Vipi kuhusu wote huko juu kwenye roshani upande wangu wa kulia? Je, kuna wengine huko juu, huku vichwa vyenu vimeinamishwa na mioyo yenu, pia, wasiomjua Bwana Yesu, useme, “Ndugu Branham, nikumbuke katika maombi yako unapoomba”? Wakristo wote upande huo? Nitawaachia sasa.

²²¹ Sasa kumbukeni, jinsi Mkristo alivyo. “Ukiipenda dunia au mambo ya ulimwengu, ni kwa sababu kumpenda Mungu hakumo ndani yako.” Hatuwezi kuchukulia jambo hili vivi hivi, ni uhalisia, ni kuzaliwa halisi, kupita halisi kutoka mautini kuingia Uzimani.

²²² Roshani upande wangu wa kushoto, kunaweza kuwako na wengine hapo uinue mkono wako, useme, “Mimi si Mkristo, Ndugu Branham, laiti ungenikumbuka katika maombi.

Simwinulii mkono wangu kama mhubiri, ninamwinulia Mungu mkono wangu, na anirehemu”? Kuna yeyote? Vema.

Chini kwenye orofa ya chini tena, hebu tupitie hapa. Kuna mwingine? Ili nitakuwa na hakika kujua ya kwamba ninaomba. Ninaamini Mungu anasikia maombi yangu.

²²³ Aliniambia, “Kama utakuwa mwaminifu, uwafanye watu wakuamini, hakuna kitu kitakachosimama mbele ya maombi yako.”

Nikasema, “Hawataniamini kwa sababu mimi sina elimu.”

Akasema, “Kama vile Musa alivyopewa ishara mbili za kuthibitisha ya kwamba alitumwa kwa ajili ya ukombozi, vivyo hivyo umepewa ishara mbili.”

²²⁴ Inua mkono wako, useme, “Ningetaka kukumbukwa katika maombi, Ndugu Branham,” kama kuna mwingine sakafuni ambaye hajainua mkono wake. Vema.

²²⁵ Baba yetu wa Mbinguni, ninawakabidhi Kwako. Kuna mikono, alasiri ya leo, iliyoinuliwa, wawili kwenye orofa ya chini, niliowaona. Sasa, Bwana, ninaomba ya kwamba utawagusa watu hao saa hii. Watu wanajisikia ya kwamba wameridhika kwamba Wewe uko pamoja nao, nami nakushukuru kwa ajili ya jambo hilo.

²²⁶ Sasa, Baba, kukiwako na kivuli kimoja cha shaka, jalia wasisimame chini ya hicho, jalia wawe na hakika kabisa, kwa sababu asubuhi hiyo itakuwa ni asubuhi mbaya sana, ukungu utakuwa mzito mtoni. Ninataka kuwa na hakika ya kwamba tiketi yangu ni sahihi, na kila kitu kimesahihishwa sasa, kwa ajili ya saa hiyo, huenda nisiwe na nafasi, sitakuwa na nafasi, hakutakuwako na rehema wakati huo. Damu itakuwa imeondolewa kwenye kiti cha rehema, kitakuwa ni Kiti cha Hukumu, nami nitaombwa kutoa jibu.

²²⁷ Mungu, jalia ya kwamba watu hawa wa thamani, ambao Wewe uligusa mioyo yao, ninaomba ya kwamba utawaokoa sasa hivi. Jalia wajue hili: ya kwamba Wewe ulisema katika Neno Lako, “Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu, asipovutwa na Baba Yangu.”

²²⁸ Nao wakainua mikono yao wakionyesha ya kwamba kulikuwa na Roho aliyewaambia wainue mikono yao. Waliinua mikono yao kuelekea Mbinguni, kwa Muumba wa Mbingu na nchi.

²²⁹ Baba, Mungu, ninaomba ya kwamba uliweke jina lao kwenye Kitabu cha Uzima. Jalia Damu ya Yesu iliandike kwenye kitabu chao cha dhambi, “Wamesamehewa,” kitupwe katika Bahari ya Usahaulifu, usizikumbuke dhidi yao tena. Na majina yao na yaandikwe upya katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo, ili katika siku hiyo, hi—hicho Kitabu kitanyunyiziwa Damu ya

Bwana Yesu, ili kusiwe na dhambi yoyote dhidi yao. Tujalie, Baba. Ninawakabidhi Kwako.

²³⁰ Nisipopata kuwapa mikono katika maisha haya, jalia nipate majaliwa hayo siku hiyo wakati hao makumi ya maelfu watakaposimama huko. Jalia niwasikie wakipaza sauti, “Ndugu Branham, mimi ndiye niliyeinua mkono wangu Yakima alasiri ile.” Watakuwa na furaha sana; lile ono uliloonyesha hivi majuzi usiku jinsi walivyokuwa na furaha, waliokuwa wamepita kutoka maisha haya hadi mengine. Sasa, Baba, ninaomba ya kwamba utawabariki.

²³¹ Sasa alasiri ya leo, tunapofanyiza mstari wa maombi, naomba ujidhihirishe Mwenyewe na kulithibitisha Neno, na uwe Mungu ndani ya watu Wake kwetu leo, tunapomwona Mungu katika ulimwengu Wake, Mungu ndani ya Mwanawe, Mungu katika Neno Lake, Mungu ndani ya watu Wake. Tujalie, Baba. Tunaomba, katika Jina la Yesu. Amina.

²³² Kwenu ninyi watu wapendwa, nilikuwa nikiwazia... Nilitoa hiyo saa. Hizo ni saa tatu mfululizo, nikishika mkono wa mtu nikiwa nimeivaa, kwa sababu hiyo, hiyo saa husimama, ilishindwa kuninii, sijui, hainiambii nini. Yule sonara mumu humu mjini, ndio kwanza aitengeneze, anajaribu kuitengeneza. Nacho kishikio kikang’oka, uso ukaanguka, mkono... Ni Kriketi ya Vulcain ya dola mia tatu niliyopewa huko Uswisi iliyo na kengele. Mnaona? Nami nilikuwa na mpya kabisa hapa California niliyopewa. Nikamwekea mtu mkono wangu namna *hiyo* kumwombea... Kuna yeyote aliyewahi kuona hilo? Aliyekuwepo wakati hilo lilipotendeka? Inueni mikono yenu, kama umekuwako, wakati hilo lilipotukia. Basi kitu hicho kilisimama, kikatengana, sijaweza kukitumia hata wa leo; saa tatu mfululizo. Niliitoa, ili niwe na hakika.

²³³ Sasa, tutaninii... Ni ipi tuliyoninii, ilikuwa, iliyoitwa jana usiku, tulipokuwa na kadi za maombi? A? A. Ulitoa nini? Kuna mia moja zilizosambazwa kwa jumla. Tuliita kutoka moja hadi hamsini, naamini, jana usiku, ndipo ikafikia ambapo hakuna mtu angekuja.

²³⁴ Sasa angalieni, najua inashangaza. Naam, bwana. Ni nzuri sana. Kama ukija hapa na dhambi isiyotubiwa, afadhali uisahihshe kabla hujaja, unaona, kwa sababu bila shaka itaitaja moja kwa moja. Lakini alasiri ya leo, nitachukua tu baadhi ya hizo kadi za maombi na kuwaombea, na halafu, kuwaombea tu watu walio na kadi za maombi.

²³⁵ Hebu tuanzie, alasiri ya leo, mahali pengine hapo ndani, kwa hiyo kama tukiwaleta watu kadhaa hapa, labda, kwa upambanuzi ama kitu fulani. Hebu tuanzie mahali pengine katika hiyo mia. Hebu tuone, tulifikia mahali fulani jana usiku kumi na tano, ama ishirini, ama kitu kama hicho, nao wakafikia mahali hata hawakuja, ndipo basi nilininii tu... .

²³⁶ Hebu tuanzie, tuseme, hamsini na moja. Je, kadi hiyo iko hapa? Hamsini na moja, ni nani aliye na kadi ya maombi hamsini na moja? Inua mkono wako. Mwanamke, vema, hapo ni pazuri kwa kuanzia. Njoo papa hapa, mama. Hamsini na mbili. Ni nani aliye na kadi ya maombi hamsini na mbili? Tutawapata wote, lakini tunaninii tu... Vema.

²³⁷ Mwanangu ananiambia ya kwamba hawawezi kusikia humu jengoni. Hiyo ni kweli? Mnaweza kunisikia huko juu kwenye roshani? Hamwezi kusikia? Mnaweza kunisikia huko? Vema, nawatakia heri, mlioketi hapa alasiri yote, wala hata hamwezi kusikia. [Ndugu fulani anasema, "Hawawezi kusikia chochote huko juu."—Mh.] Hawawezi kusikia hata jambo moja kwenye roshani. Mna—mnaweza kusikia huko nyuma? Wanaweza kusikia huko nyuma, bali hawawezi kusikia huko juu kwenye roshani. Mbona, naitakia heri mioyo yenu miaminifu! Mungu, Mwokozi wangu, na awajalie haja yenu, kila mmoja wenu, alasiri ya leo. Mnaweza kusikia hilo? Mungu na awajalie haja yenu, chochote ilicho, kama mliketi hapo wakati huu wote, nami nikizungumza, wala msingeweza kusikia chochote. Mungu na awafunulie hilo kwa njia nyingine, kwamba mimi, ninawaambia kweli.

²³⁸ Vema, tutaitisha mstari wa maombi sasa. Itanibidi kulisema kwa sauti kubwa namna hii, kwa sababu watu huko juu huenda wana kadi za maombi. Ninaita kutoka kwenye kadi ya maombi... Nilikuwa wapi? [Ndugu mmoja anasema, "Hamsini na mbili."—Mh.] Hamsini—... Kadi ya maombi hamsini na mbili. Vema, kadi ya maombi hamsini na mbili, ni nani aliye nayo? Hamsini na tatu. Njoo papa hapa, mama. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

²³⁹ "Bwana Yesu, waweza kuniponya?"

Angesema, "Ewe mtoto, tayari nimefanya hivyo."

"Vema, ati tayari umeniponya? Sasa, ngoja kidogo, hiyo ni ninii kidogo... nilisikia Wewe ni Mponyaji."

"Mimi ni Mponyaji," Yeye angesema.

"Vema—vema, kwa nini usiniponye?"

²⁴⁰ "Mbona, ewe mtoto, tayari nimefanya hivyo. Nililipa gharama ya uponyaji wako kule nyuma. Siwezi kamwe, kamwe katika siku Zangu nilipokuwa duniani, wala siwezi sasa, wakati wowote, kufanya lolote kwa ajili ya mtu yeyote, isipokuwa wawe na imani ya kuliadini kwanza."

Ni wangapi wanaojua hilo? Huo ndio msingi, haina budi kuwa ni imani. Vema.

Sasa, wangesema, "Vema, ninajuaje Wewe ni Bwana Yesu? Waweza kufanya jambo fulani?"

"Mbona, naam, nitainua mkono Wangu, nitahubiri kitambo kidogo."

Lakini unaona, useme, “Bwana, jalia nijue ya kwamba ni Wewe.”

²⁴¹ Ingembidi kufanya jambo kama alivyofanya alipokuwa hapa duniani. Hiyo ni kweli? Kufanya jambo fulani kukufanya ujue. Basi ni ishara gani tuliyoipata jana usiku ambapo aliwafanya watu wajue ya kwamba Yeye alikuwa ndiye Masihi? Alifanyaje jambo hilo? Alikuwa amewapa ishara ya Masihi kuonyesha ya kwamba Yeye alikuwa ni Nabii ambaye Musa alinena habari zake, Alijua siri ya mioyo yao. Ni wangapi wanaojua hilo? Ni mashahidi wangapi ambao Biblia inasema ya kwamba, “Ya kwamba Bwana, Mungu wenu, atawaondokeshea Nabii kama nilivyo mimi”? Naye Yesu alijua mawazo yao, alijua siri za mioyo yao, akawaambia, na katika hilo, Yeye alijidhihirisha Mwenyewe kuwa Mwana wa Mungu.

²⁴² Sasa, kama Mungu yuko ndani ya watu Wake, Uhai ule ule uliokuwa ndani ya Yesu, uko hapa ndani ya Kanisa, na yako ndani yenu enyi watu. Mwanamke huyo akipenyeza kupitia kwenye mstari wa maombi, hakuwa na kadi ya maombi, kama vile tungenema, bali alikaa huko nyuma kwenye kusanyiko, akagusa upindo wa vazi Lake.

²⁴³ Sasa Yesu, leo, ni Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu. Hiyo ni kweli? Sasa, ungejua je ulingusa? Angetenda vile vile alivyotenda alipokuwa hapa.

²⁴⁴ Sasa, mara nyingi, ninyi watu mliolemaa, na kadhalika, mngewazia, “Nimepoteza matumaini kabisa.” Ondoa hilo akilini mwako. Hakuna zaidi kwa Mungu kwako kupokea imani kuliko ilivyo kwao kupokea imani. Uponyaji wako ni wa hakika tu kadiri wao ungekuwa, iwapo, uponyaji wako ni wa hakika tu iwapo utakuwa na imani.

Sasa, ni ipi . . . ? Tuanzie wapi? Papa hapa kwa mama huyu. Vema. Njoo hapa.

²⁴⁵ Sasa, Wamarekani, sasa, tunatambua kwa watu hamsini, mimi, wangenibeba waniondoo jukwaani baada ya kumi au kumi na watano kupita kwa kwa ajili ya maono. Mbona, nisingeweza kustahimili jambo hilo. Ni wangapi wanaelewa hilo? Yesu kwa ono moja, nguvu zilimtoka. Na sasa, ono moja lingenifanyia nini mimi?

²⁴⁶ Sasa, huyu hapa mwanamke kiwete kwenye kiti cha magurudumu. Ninasema, “Mwanamke huyo ni kiwete,” mtu yeyote anajua hilo. Lakini huyu hapa mwanamke anayeonekana mwenye afya. Sasa mwujiza ni kwamba, ana shida gani? Anaonekana mzima na mwenye afya, Sasa, kama mtu yeyote ana shaka juu ya jambo hili, na kuwazia ya kwamba—ya kwamba una njia bora zaidi, mbona, hii *hapa* maikrofoni, njoo moja kwa moja hapa juu. Mna—mnakaribishwa tu kuja. Ninyi ambao ha—hamwamini, njoni hapa juu na kufanya jambo lile lile.

Mnasema, “Vema . . .”

Yesu alisema, “Kazi nizifanyazo Mimi, ninyi nanyi mtazifanya, kubwa zaidi.”

“Vema,” mlisema, “Alisema *kubwa* zaidi.”

²⁴⁷ Vema, hebu tukuone kwanza ukifanya kazi alizofanya, kisha ufanye kubwa zaidi. Wewe fanya kazi za kwanza alizofanya, ndivyo hivyo, ndipo ninyi—ndipo nyinyi mtafanya makubwa zaidi. Unaona? Hebu tukuone ukifanya mambo ya kwanza aliyofanya. “Kazi nizifanyazo Mimi, yeye naye atazifanya,” basi kubwa zaidi. Kama utachukua tafsiri, inasema, “Nyingi kuliko hizi atafanya,” maana asingeweza kufanya kubwa zaidi, maana Yeye—Yeye alifanya karibu kila kitu ambacho kingeweza kufanywa.

²⁴⁸ Lakini sasa, kama mwanamke huyu... Sasa, nitawaombea tu hao watu wengine huko chini mstarini. Lakini huenda watu wakajua ya kwamba Roho Mtakatifu yupo hapa, sasa nitaona kama Mungu atatupa ono kwa ajili ya mwanamke huyu.

²⁴⁹ Sasa, aliponiambia ishara hizi mbili zitathibitisha ya kwamba ulitumwa kufanya jambo hili, Musa alikuwa na ishara mbili, Yeye alisema. Musa alishuka akaenda kule na kufanya ishara wakati mmoja mbele ya Israeli, ndipo kila mtu akamwamini na kwenda kwa miguu miaka arobaini. Hiyo ni kweli? Hakika, kama sisi ni wana wa Ibrahimu moyoni, tunapaswa kuwa na imani kiasi hicho. Sasa hebu na tuamini.

²⁵⁰ Sasa, mama, kwanza kabisa, nadhani hatufahamiani. Kama hatufahamiani, waweza tu kuinua mkono wako kusudi watu waone?

²⁵¹ Sasa, mnaona, sisi hapa, sio huko nyuma kwenye kona fulani yenye giza kama ibilisi, papa hapa nje, kama vile Bwana wetu alivyosimama, kama yule mwanamke kisimani. Kamwe usiuogope Ukristo, ning'iniza nafsi yako kwenye ahadi yoyote, ni ya kweli, Kristo alikufa apate kuitimiza.

²⁵² Sasa, kamwe nisingesema hilo, kama sikuuhisi Uwepo Wake hapa, kama vile yule tai alivyoyahisi mabawa yake. Mnaona?

²⁵³ Sasa, huyu mwanamke, tangu amekuwa akisimama hapa, ametambua ya kwamba yuko Mbele ya *Kitu fulani* mbali na mwanadamu. Hiyo ni kweli, mama? Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako.

²⁵⁴ Mnaona, kimesimama papa hapa juu ya mwanamke huyu, kama ninyi, macho yenu ni ya kiroho, hakika mnaweza kukiona. Hivi hamwoni hiyo Nuru inayoning'inia papa hapa? Moja kwa moja juu ya huyu mwanamke. Kwa namna fulani ni ya zumaridi. Ni wangapi wameiona, ile picha yake? Iko hapa mkutanoni, wanayo. Imetundikwa huko Washington, DC, ndicho Kiumbe pekee cha kimbinguni kilichowahi, kilichowahi kupigwa picha ikathibitishwa, kisayansi. Hii hapa, ninaiangalia moja kwa moja. Imening'inia juu ya huyu mwanamke, maana yeye ni

mwaminio, yeye ni dada yangu, Roho anashuhudia huku na huku.

²⁵⁵ Sasa, jambo pekee ninalopaswa kufanya ni kushika tu kitu fulani kutoka kwake. Ndipo nini kingetukia? Ingemwambia jambo fulani. Ama amesimama hapa kwa ajili ya tatizo la kinyumbani, tatizo la kifedha, ugonjwa, au mtu mwingine, ama chochote kile. Sijui, sijawahi kumwona maishani mwangu.

Sasa, kama Roho Mtakatifu atamfunulia huyu mwanamke jambo fulani kuninii... Sasa, kama ningesema, “Naam, Yesu Kristo yupo hapa, nilihisi Uwepo Wake.” Yeye anauhisi, pia.

²⁵⁶ Sasa angalia jinsi ilivyo. Ni hisia tamu sana, nyenyekevu, pole. Hiyo ni kweli, mama? Kama ndivyo, wapungie wasikilizaji mkono wako mbele na nyuma. Unaona? Ninaiangalia ile Nuru moja kwa moja juu yake. Sasa, kwangu mimi, najua ninalizungumzia kusanyiko, lakini kwa kweli akili yangu, inaonekana, iko katika ulimwengu mwingine, iko katika kiwango fulani, ulimwengu mwingine.

²⁵⁷ Huyu Mama ana shida, iko kifuni mwake, ni vivimbe, ni vivimbe vya kansa. Amefanyiwa upasuaji, ama kitu fulani, kwa ajili yake. Navyo vina—vinarudi, vivimbe kifuni mwake, ambavyo hatimaye vitamwua huyu mwanamke, ametiwa uvuli wa mauti. Kama hiyo ni kweli, mama, pungu mkono wako.

²⁵⁸ Sasa, unaamini? Sasa, kwa kuwa huenda mnajua, angalieni nguvu za ibilisi zikifanya kazi, mwanamke huyu, kwa kweli kwenye hili hapa, wakati ningali katika roho, ni kitu kama uvimbe. Hiyo ni kweli? Papa hapa ameketi mtu mwingine, mwanamke aliyekei papa hapa akiwa na uvimbe. Hiyo ni kweli, mama? Kama ndiyo inua mkono wako. Lakini mbali na hayo, una kisukari pia. Hiyo ni... Inua mkono wako.

²⁵⁹ Unaona? Roho huyo wa giza akivuka hapa, hao pepo wawili wakijaribu kushikana, wakiomba usaidizi. Lakini nguvu za Mungu sasa, juu ya kila shaka humu ndani hazina budi kushinda shaka. Unaona?

Sasa, unaamini? Je, Mungu yuko ndani ya watu Wake?

Unasema, “Mungu yuko ndani yako, Ndugu Branham?”

²⁶⁰ Sio mimi tu, yuko ndani *yake*, na ndani *yake*, pia. Mnaona? Huyu hapa Roho Mtakatifu hapa, ambaye hakosei, kuna nguvu za mauti katika wote wawili na hivyo vifo viwili vinajaribu kushirikiana pamoja, huku nguvu za Mungu zikifunua hilo, akilifungua na kuonyesha ya kwamba anawapenda hao wanawake, Anataka waponywe. Mnaamini hilo?

²⁶¹ Sasa, tafadhali, tafadhali msisogee huku na huku. Sasa, mlivunja mkondo wake wenyewe, mnaona. Msifanye hivyo, tafadhali, tafadhali. Mnajua vitu hivi vitatoka kwa mmoja vimwendee mwingine? Iweni na kicho kabisa, kila mtu.

²⁶² Mama, kama Mungu angeniambia wewe ni nani, ingekupa imani kubwa ya kuamini? Jina lako ni Bi. Moore. Nendeni zenu, nyote wawili, aliwaacha nyote wawili papo hapo, mmeponywa, nendeni zenu na mpate afya.

Hebu tuseme, “Bwana asifiwe.” Je, karama hiyo inafanya kazi?

²⁶³ Sasa, ni wangapi wanaokumbuka nilipokuwa hapa wakati nilipomwekea mtu fulani mkono wangu, nawe ungeona ni—nini, kama mtetemo juu yake? Sasa, kama mwanamke huyu ana ugonjwa wa viini, itafanya kazi. Kama si ugonjwa wa viini, haitafanya kazi, maana itabidi ionekane kwa ono. Sijui.

²⁶⁴ Wewe ndiye mgonjwa anayefuata? Sijarukwa na akili, lakini ni kwamba tu wakati mwingine mimi . . . Njoo hapa kwa dakika moja, ewe msichana. Hebu niushike mkono wako kwa muda kidogo tu, mkono huu papa *hapa*. Kweli, ni ugonjwa wa viini. Naam, bwana. Ana maambukizo. Sasa, ni ugonjwa wa kina mama, ugonjwa wa kike. Hiyo ni kweli. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Hiyo ni kweli kabisa. Mnaona? Ana maambukizo, hiyo ni seli hai; hii hapa kwenye mkono wangu.

²⁶⁵ Ninataka kukuonyesha jambo fulani, ewe msichana. Angalia hapa, angalia mkono wangu. Unaona vitu hivyo vidogo vyeupe vinavyoruka juu ya mkono wangu pale, kidogo vilivyovimba, vyenye rangi nzito, vinavyoonekana vyekundu? Sasa ondoa mkono wako kutoka kwa wangu. Sasa havipo sasa. Sasa weka mkono huu *hapa* juu yake. Havipo sasa. Havipo sasa. Sasa weka mkono *huu* hapa juu yake. Hivyo hapo.

²⁶⁶ Sasa, wewe ni mwanadamu tu katika mkono *huo* kadiri ulivyo katika mkono *huu*, nami ni mwanadamu tu kadiri wewe ungekuwa mwanadamu, lakini haitafanya kazi *hapa*, haitafanya kazi *hapo*, kwa sababu Mungu aliniambia, katika ono, “Kusudi watu wajue ni kweli, mchukue mtu huyo, acha wao . . .” Unaona? Unapoweka mkono wako wa kuume kwangu, unaahidi kwamba unaniamini. Yeye alisema, “Kama unaweza kuwafanya watu wakuamini, na uwe mnyofu, hakuna kitu kitakachosimama mele ya hayo maombi.”

²⁶⁷ Je, mliwahi kukisoma hicho kitabu? Ni wangapi wamesoma hayo katika vitabu? Kwa miaka na miaka . . . Sasa, mnaona, basi nitakupa mkono wangu wa kushoto kwa sababu wewe ni dada yangu tu, wangu wa kulia unaenda kwa Mungu, ninaamini ahadi Yake kwamba aliniambia hivyo. Mnaona? Ndipo unasema, “Ninaamini.” Kwa nini? Kwa sababu isingekuwa sana sana ni mhemuko mkononi mwangu, kama kuwaambia kuna shida gani. Basi unaniamini, sivyo? Kisha ninamwinulia Mungu mkono wangu, “Ninakuamini, Mungu.” Niweke mkono wangu *hapa*, “Mimi,” wewe, “ninakuamini, Ndugu Branham.” Hilo hapo. Unaona? Hilo hufanya hivyo.

268 Sasa, weka mkono wako *hapa*. Sasa, nataka uone, ewe msichana, ya kwamba si jinsi ninavyoweke mkono wangu, ama ninii yoyote. . . Vema, jambo lenyewe ni kwamba, ningejua je ilikuwa ni nini, kama haikuwa hivyo? Lakini unaona kuna msisimko mkononi mwangu pale, sivyo? Vitu vidogo vyeupe, vikipita juu ya mkono wangu. Sasa, mara tu unaposogeza mkono wako, vinaondoka. Wala hakitakuja kwa mkono huu mwingine. Sasa nimeuweka *hapa*, hicho hapo tena. Unaona?

269 Sasa angalia, mama, ninataka uangalie hilo kwa makini sana, kama hicho kikitoweka, umeponywa. Lakini sasa kumbuka, sitaweza kukizuia, kwa sababu, “Pepo mchafu anapomtoka mtu, anatembea mahali pasipo na maji, anarudi pamoja na pepo wengine saba.”

270 Vema. Kama Mungu anaweza kuja hapa na kukuonyesha jambo fulani, dhahiri, nawe unajua bila shaka yoyote kwamba jambo fulani linatukia, na kuna Mtu fulani hapa anayekujua (Hiyo ni kweli?), katika Roho. Kitu fulani kilitambua ugonjwa uliokuwa nao.

271 Sasa, huo ukiondoka, je, utaamini utakaa hivyo? Vema. Ninyi wanawake, nyote inamisheni vichwa vyenu kwa dakika moja tu. Ninawatakeni muuangelie mkono wangu. Sasa, kwanza nitaomba. Chunguza tu imani yako, nami nitakuonyesha ya kwamba sitapoteza mkono wangu.

272 Baba yetu wa Mbinguni, ninamwomba msichana huyu, ya kwamba utaondoa mateso haya mwilini mwake. Wewe ni Mungu, mkono wangu umewekwa hapa kando ya Biblia Yako. Uliahidi kuwaponya wagonjwa, hilo ni Neno Lako. Tunakuamini kwa yote yaliyo moyoni mwetu. Sasa, jalia hicho kitu kimwache, Baba. Ninaomba, kupitia Jina la Yesu.

273 Sasa, kabla sijainua kichwa changu, kitu hicho hakijaondoka. Hiyo ni kweli, mama? Sema—sema, “Ndiyo au la.” Kingali pale, sivyo? [Mama huyo anasema, “Ndiyo.”—Mh.] Naam, kingali kinasonga mbele. Mnaona? Maombi tu peke yake, hayatafanya hivyo, haina budi kuchukua imani. Unaona ninalomaanisha sasa?

Sasa angalia, hicho hapo tena. Sasa, unaamini ya kwamba Biblia ilisema, “Katika Jina Langu watatoa pepo?”

274 Sasa, inakubidi kuangalia kile unachofanya kuhusu hilo. Inakubidi kuangalia, kwa sababu kumbuka, Musa alipiga mwamba wakati hakupaswa kuupiga; Eliya aliwalaani watoto wadogo arobaini na wawili, naye dubu akawaua kabla hawajarudi, kwa sababu walisema alikuwa na upara, wakimtania kuhusu hilo. Haikuwa ni mapenzi ya Mungu kufanya hivyo, hilo halisikiki kama Roho Mtakatifu, nabii mwenye hasira.

275 Sasa, ninataka uangalie ni—ninii, msichana, wewe angalia mkono wangu. Kuwa mwaminifu, unaona. Sasa, kama mkono huo ukigeuka nyuma namna *hii*, vimekwisha bila mimi kusogea.

276 Sasa inamisha kichwa chako kila mahali, maana huna budi kukifanya kiondoke sasa. Ukikifanya kiondoke, kinakasirika, nasi tunajua kitatoka kwa mmoja kimwendee mwingine.

277 Ewe Shetani, Malaika wa Mungu alikuja miaka kumi na minne iliyopita kwenye Kinu cha Green, usiku mmoja, na kuniambia, kama mhudumu wa mahali hapo kwamba nilitumwa kuwaombea wagonjwa, na haya ndiyo yaliyosemwa. Unajua jambo hilo, umefichuliwa. Unaweza kuwa na kutokuamini ndani ya watu, unaweza kuwafanya watu washuku, bali huwezi kumfanya Kristo afanye lolote, kwa sababu amekunyang'anya kila haki ya kisheria uliyowahi kuwa nayo. Alipokufa pale Kalvari, alilipa deni ya dhambi zetu zote na kutokuamini.

278 Mungu amewapa watumishi Wake nguvu za kukutoa. Ninalitumia Jina Lake, ninakuja katika Jina la Yesu Kristo. Ninakupa changamoto katika pambano hili la imani, mwache msichana huyu, toka ndani yake, katika Jina la Yesu Kristo!

279 Sasa, kabla sijainua kichwa changu, kufungua macho yangu, kitu hicho kimeondoka. Hiyo ni kweli? Sasa fungueni macho yenu. Jambo fulani lilitukia, sivyo? Hata unajisikia tofauti, sivyo? Sasa, angalia *hapa*. Hilo hapo. Sasa ngoja, nitaondoa mkono wangu kwako. Sasa weka mkono *huu*, kama tu ulivyofanya muda mfupi uliopita. Unaona jinsi unavyoonekana? Sasa, weka mkono *huu*, kama tu ulivyofanya muda mfupi uliopita. Unaona jinsi unavyoonekana? Jambo fulani lilitukia, sivyo? Umeponywa. Hivyo ndivyo ilivyo, hivyo tu. Nenda zako ukishangilia, ukisema, “Asante.”

280 Sasa, hebu tuone mkono wa mwanamune huyu kwa dakika moja tu. Ana tezi kibofu kidogo kinachomfanya awe na wasiwasi kuamka, ama chochote kile. Lakini, hilo ni sawa, unaamka usiku, lakini hilo silo unalotaka hasa, kwa sababu ninahisi roho yako ikisogeza kitu kingine. Vema. Unafikiri ungewahi kuwa kiwete? Unafikiri yabisi kavu hiyo ingeweza kukulemaza, ama chochote kile? Unaamini Mungu atakuponya sasa? [Ndugu huyo anasema, “Ninajua Mungu ataniponya.”—Mh.] Amina. Amekuponya. Ondoka jukwaani ukishangilia, na kupaza sauti, ukisema, “Bwana asifiwe.”

Hebu tukuone, bwana, njoo hapa kwa dakika moja. Hebu nishike mkono wako. Naam, bwana, ugonjwa wa tumbo. Unaamini Mungu atakuponya huo?

Katika Jina la Yesu Kristo, ibilisi na amwache mvulana huyu. Toka ndani yake, katika Jina la Yesu. Amina.

Nenda, amini.

Vema. Njoo. Kwa ajili ya mtoto mchanga? Sasa, hebu na tuone maskini mkono wake sasa. Hebu kidogo.

U hali gani, mvulana mdogo? Halo hapo, jamani. Naam, bwana.

²⁸¹ La, sivyo, si maambukizi. Hebu kidogo. Sasa, unaamini kama Mungu anaweza kuniambia mtoto huyu ana shida gani, kwamba Mungu atamponya? Je, utamkubali Yesu kama Mponyaji wa mtoto huyo mchanga? Ni ugonjwa wa moyo, ni moyo mbaya. Madaktari hata hawajui la kufanya kulihusu. Hiyo ni kweli. Lakini Mungu anajua la kufanya juu yake.

Shetani, mwache huyo mtoto!

Katika Jina la Yesu, ninamhukumu ibilisi, ninaomba kwa ajili ya uponyaji wake. Amina.

Mchukue sasa. Amini kwa moyo wako wote, atapona.

²⁸² Njoo. U hali gani, mpenzi? Unamwamini Yesu? Hebu tuone maskini mkono wake. Sasa, naam. Unafikiri huo ugonjwa wa figo utaondoka, nao watapata afya, na kuwa wazima? Unaamini kwa moyo wako wote kwamba Kristo atamponya?

²⁸³ Bwana Yesu, ninamhukumu ibilisi ambaye amemdhuru mtoto huyu, jalia aondoke, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

²⁸⁴ Kuwa na imani, amini sasa, usiwe na shaka. Nenda, ukiamini, na kama ukiamini kwa moyo wako wote, itatukia.

Sasa, hebu tuone mkono wako. Ugonjwa wa pumu, lakini unaamini ya kwamba Mungu angeweza kuuponya huo, kuufanya mzima? Je, utamkubali kama Mponyaji wako?

Ninamhukumu ibilisi ambaye amemdhuru dada yetu. Katika Jina la Yesu Kristo, mwache mwanamke huyu!

Nenda, ukiamini sasa, usiwe na shaka, bali amini kwa moyo wako wote.

Ni wangapi huko nje, ambao hawana kadi za maombi, wataamini? Ni wangapi wenu watakaosema kweli, "Ninaamini"? Kuwa na imani, usiwe na shaka.

²⁸⁵ Unaamini hiyo yabisi kavu itakuacha? Huyu mtu aliyeketi hapo akiniangalia, papa hapa nyuma, mtu anayeonekana mzee. Kama ukiamini kwa moyo wako wote, Mungu atakuponya.

²⁸⁶ Huyu hapa ameketi mwanamume, papa hapa, akiwa na henia. Unaamini Mungu atakuponya, bwana? Uliyeketi papo hapo ukiwa na henia, ukiomba. Wewe ambaye kidogo una upara hapa mbele, uliye na tai ya kamba. Naam, bwana. Simama kwa miguu yako na ukubali uponyaji wako basi. Je, una kadi ya maombi? La, bwana. Mke wako ana moja. Vema, kama mke wako ana moja, huna moja basi. Unaweza kwenda naye nyumbani, na aponywe, kama ameponywa mstarini. Amina.

Kama utaamini kwa moyo wako wote! Ninawapa changamoto kuamini kwamba ni kweli. Mnaamini, kila mmoja wenu? Basi mwaminini Mungu.

Jambo fulani lilitukia, mahali fulani. Haikuwa ni mtu huyu. Unaamini Mungu atakuponya?

Bwana, katika Jina la Yesu, mponye mwanamke huyu. Amina.

Sasa, nenda ukaamini kwa moyo wako wote. Kama unaweza kuamini jambo hili, wala usilitilie shaka, litatukia.

²⁸⁷ Njoo, dada. Sasa, unajua ninajua shida yako. Lakini, kama ni—kama nisipokwambia, wewe amini, kwa vyovyote vile, sivyo? Naam, bwana. Lakini nitakwambia tu, wasiwasi wako umekuondokea, unaweza kwenda nyumbani, uwe mzima. Amina. Kwa hiyo usiwe na shaka sasa.

Ulipokuwa umeketi pale ugonjwa wa moyo uliondoka, kwa hiyo endelea tu kutembea, ukisema, “Asante, Bwana.” Unaona? Unaona?

²⁸⁸ Sasa, nisipokwambia jambo moja, utakubali, na kuamini ni sawa? Vema, ugonjwa wako wa mgongo umekwisha, kwa hiyo nenda tu nyumbani ukapate afya. Na u—umwamini Mungu, amini kwa yote, moyo wako wote.

Bwana Yesu, ninaomba ya kwamba utamponya mwanamke huyu, katika Jina la Yesu.

Njoo sasa, ukiamini kwa moyo wako wote.

Katika Jina la Yesu, ndugu yetu na aponywe.

²⁸⁹ Sasa, mnaona wanaponywa vivyo hivyo. Unaamini hilo?

Njoo dada.

Katika Jina la Yesu Kristo, dada yetu na aponywe.

Amini, usiwe na shaka.

Tunamwona maskini ndugu huyo amelemaa. Unaamini ya kwamba Mungu atakuponya, bwana?

Katika Jina la Yesu Kristo, ndugu yetu na aponywe. Amina.

Usiwe na shaka, nenda ukiamini sasa, utapona.

Njoo bwana.

Katika Jina la Yesu Kristo, ninaweka mikono yangu juu yako, ndugu, nayo Biblia ilisema, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Amina. Katika Jina la Yesu, uponywe.

Unaamini, dada?

Katika Jina la Yesu Kristo, jalia waponywe. Amina.

Sitafuti maono kwa sababu ninadhoofika sana sasa, mpaka ninahisi tu miguu yangu ikitetemeka chini yangu.

Katika Jina la Yesu Kristo, jalia waponywe.

Unaamini sasa, sivyo?

Utaamini?

Katika Jina la Yesu Kristo, jalia waponywe. Amina.

Njoo, maskini mama. Utaamini?

Katika Jina la Yesu Kristo, dada na aponywe.

Katika Jina la Yesu Kristo, dada yetu na aponywe.

Njoo, ndugu. Utaamini hili sasa, sivyo?

Katika Jina la Yesu Kristo, ndugu yetu na aponywe.

Njoo, dada. Bila shaka unajua ninii yako...?...

Katika Jina la Yesu Kristo, dada yetu na aponywe.

Katika Jina la Yesu Kristo, dada yetu na aponywe.

Katika Jina la Yesu Kristo, dada yetu na aponywe.

Katika Jina la Yesu Kristo, dada yetu na aponywe.

Katika Jina la Yesu Kristo, ndugu yetu na aponywe.

Mungu akubariki, ndugu.

Katika Jina la Yesu Kristo, naomba uponywe.

Njoo, dada.

Katika Jina la Yesu Kristo, jalia aponywe.

Katika Jina la Yesu Kristo, jalia aponywe.

Njoo, ndugu. Amini sasa, nao utakuacha.

Katika Jina la Yesu Kristo, ndugu yangu na aponywe.

Katika Jina la Yesu Kristo, ndugu yangu na aponywe.

Njoo, ndugu.

Katika Jina la Yesu Kristo, ndugu yangu na aponywe.

²⁹⁰ Unatilia shaka? Je, una—una—unatilia shaka kwa moyo wako wote? Ama je, unaamini kwa moyo wako wote? Unaamini? Sasa, kamwe sikutumia upambanuzi. Nilijua shida ya watu. Mnajua hilo, sivyo? Hapa. Je, huyu...? Ningali nina yule mgonjwa mkononi mwangu.

²⁹¹ Angalia hapa, bwana, ndiyo kwanza niseme, “Mungu akubariki.” Hayo ndiyo yote niliyosema, na kuendelea. [Ndugu huyo anasema, “Amina.”—Mh.] Hiyo ni kweli? Unaamini umeponywa, kwa vyovyote vile? [“Amina.”] Vema. Ulikuwa na kansa. [“Hiyo ni kweli.”] Na hiyo ilikuwa kwenye mfupa wa nyonga. [“Hiyo ni kweli.”] Jina lako ni Bw. Peterson. [“Hiyo ni kweli.”] Nenda nyumbani, ukaponywe.

Mnaona? Mnaona? Jambo ndilo hilo. Amini tu.

²⁹² Unayeketi papo hapo na ukurutu. Unaamini Mungu atakuponya, akupe afya? Una kadi ya maombi? Huna. Unaamini ya kwamba Mungu atakuponya, hata hivyo? Vema, pokea uponyaji wako. Yesu Kristo anakuponya. Amina.

²⁹³ Mnaamini kwa moyo wenu wote, kila mmoja wenu? Ni wangapi wanaoamini ya kwamba Mungu yuko katika ulimwengu Wake? Mungu yuko katika Neno Lake? Mungu yuko ndani ya Mwanawe? Mungu yuko ndani ya watu Wake?

²⁹⁴ Sasa, ni wangapi wanaojisikia ya kwamba una Mungu moyoni mwako? Inua mkono wako. Vema. Sasa wekeaneni mikono, na mwe mkiombeana, ninaposhuka, niwaombee watu hawa kwenye kiti cha magurudumu.

Ndugu Roy, waongoze katika maombi huku wewe . . .

²⁹⁵ Wekeaneni mikono, wekeaneni tu mikono. Amini kwa moyo wako wote.

²⁹⁶ Bwana Yesu, njoo sasa, Wewe uko hapa pamoja na watu. Mungu yuko ndani ya watu Wake. Jalia waponywe, kila mmoja wao.

²⁹⁷ Wakati tukiwa katika maombi, wekeaneni mikono, endeleeni kuomba. Mungu yuko ndani ya watu Wake. Aminini, ninapowaombea hawa. 

60-0731 Tuonyeshe Baba Itatutosha
Eisenhower High School
Yakima, Washington Marekani

SWAHILI

©2025 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org